# Mahali Pekee Palipowekwa na Mungu Pa Kuabudia

Shreveport, Louisiana USA

Novemba 28, 1965A

1 Habari za asubuhi! Nina furaha kuwa hapa asubuhi ya leo. Nasi tuna furaha, tukifurahia ushirika huu mkuu kwenye nyimbo hizi za kale za imani. Tunapenda jambo hilo. Sivyo? Pambio ya *Amina*. Hivyo ndivyo Yeye alivyo, Amina, mnaona. Yeye ana neno la mwisho kusema.

Nilikuwa nimeketi pale nikizungumza na rafiki yangu wa zamani, Ndugu Brown, wakati nyimbo zilipokuwa zikiendelea. Naye akasema, "Ndugu Branham, kamwe sikuwa nimeona mpaka jana, yale umekuwa ukizungumzia." Akasema, "Kama watu wangaliingia tu kwenye yale unayozungumzia," kasema, "kila kizuizi kingeondolewa." Hiyo ni kweli kabisa. Hiyo ni kweli. Ni kweli kabisa. Kama ungaliweza tu kulishika kwa kikamilifu, ungeweza kulishika. Mnaona?

2 Nikizungumza na maskini rafiki yangu, Ernie Fandler. Nadhani baadhi yenu huko nje kwenye mahojiano mtamkumbuka Ernie, namna alivyoongoka, namna alivyoongozwa kwa Bwana. Yeye hazungumzi Kiingereza kizuri, ama ningetaka aje aseme neno. Naye huzichanganga sisi na S zake kabisa. Alikuwa akiniuliza endapo ninakumbuka ule wakati huko Shawano ambako anaishi. Kulikuwako na mtu aliyekufia moja kwa moja mkutanoni, akaanguka kitini mwake akafa, Mlutheri. Tulimfanya kila mtu anyamaze. Kanena Neno la Bwana juu yake, akawa hai, na akarudi moja kwa moja kazini. Um-hum. Hawajapata kusahau hilo, wanatutaka turudi tena.

3 Nilisikia ya kwamba huko Ufaransa, asubuhi ya leo, kuna zaidi ya Wafaransa elfu mbili wanaofunga kwa siku kadhaa ya kwamba tutakuja kuuleta Ujumbe Ufaransa katika Kifaransa. Taifa zima la Kiprotestanti, sehemu ya Kiprotestanti ya taifa la Ufaransa. Na kwa hiyo sisi ni …

Imeanza tu kuchanua sasa, kumeanza tu, makapi yanaanza kuondoka kusudi ngano iweze kukaa kule nje sasa. Mnaona? Kwa hiyo endeleeni tu kuwa na kicho, endeleeni kuomba. Mnaona? Kumbukeni, "Wao wamngojeao Bwana, wanapata nguvu mpya."

Sasa, kuna … Nilikuwa…ninazeeka sana, nami niliwazia, "Je! mimi ... Je! Kutakuwako na ufufuo mwingine, nitakaouona wakati mwingine?" Na kumbukeni tu, kutoka magharibi atakuja mpanda farasi mweupe. Tutapitia njia hii tena. Hiyo ni kweli. Mara tu tunapokuwa tayari. Ni ahadi, mnaona.

4 Sasa, nataka kumwambia Ndugu Leo … Nilikuwa nikizungumza juu ya Ndugu Wood jana usiku, ndugu yake akiwa hapa. Ndugu Leo, kama wewe na kundi dogo lililounganishwa kule juu asubuhi ya leo; Dada Mercier, baba yako yuko hapa. Nilimwona jana usiku. Yeye yuko hapa kwenye jengo mahali fulani, naye anaonekana mzuri na wala hana neno.

Ile asubuhi aliyoponywa kule hekaluni, kulikuwako na magonjwa mawili makubwa ya kansa, wakifa kweli, na yote mawili yaliponywa. Naye baba yake, mzee katika ugonjwa wa moyo, aliponywa kwa utukufu wa Mungu. Naye yuko mkutanoni hapa mahali fulani. Siwezi kumwona miongoni mwa umati sasa, bali alikuwa hapa jana usiku.

5 Salamu kwenu nyote kote nchini; hapa katika mahali hapa pazuri sana, pa Maskani ya Uzima hapa Shreveport, pamoja na umati uliosongamana kwa ajili ya shule ya Jumapili. Mwajua, kama niliishi Shreveport, bila kusema neno dhidi ya mtu ye yote, bali hapa ndipo mahali ningekuja kanisani, papa hapa kwenye Maskani ya Uzima. Hili si dhehebu. Maskani ya Uzima, leo hii, ni maskani yenye madhehebu mbalimbali. Walitoka kwenye madhehebu kwa sababu walinikubali mimi na Ujumbe huu ninaohubiri. Ndugu Jack Moore, ndugu yangu na rafiki yangu, yeye aliondolewa kwenye madhehebu kwa sababu alishirikiana nami. Na kwa hiyo nafikiri anastahili sifa. Hiyo ni kweli. Mungu ambariki. Na kuinua mikono yake katika maombi, na kuamini pamoja naye.

6 Na sasa Dada Moore, simwoni popote, yeye, naam, hapa nyuma, anaonekana kama msichana mdogo anayeketi pale asubuhi ya leo, amevalia nadhifu, mpya, katika hili, anaonekana kama mavazi ya Pasaka. Na inaonekana … Ndugu Jack mwenyewe hata hakumtambua. Sasa, sasa Dada Moore!

Hakika tunawakosa Anna Jeanne na Don, na hao wote. Ninafurahi kukutana na Ndugu Nolan, yule … mmoja wa washirika hapa.

7 Na Ndugu Ernie, nilimwuliza jana kama angeuimba huo *Amina*. Ninao kwenye santuri, nami nimekimaliza kitu hicho kwa kuusikiliza tena na tena, Amina. Nafikiri ana sauti kwa ajili ya huo; anashinda yeyote wao. Na maskini Judy, nilimwona; hayo mawili, wanaonekana tu kama kaka na dada. Sivyo? Wao ni mume na mke. Mwangalieni kila mmoja wao, mwone ni kwa nini wanafanana kabisa. Mnaona? Na kweli ni wanandoa wadogo wanaopendeza. Hiyo ni, mwajua, hiyo ni … Ndugu Palmer ambaye ndiyo kwanza apande vile vipandiyo vya dhahabu, huyo ni binti yake na mkwewe. Na huyo ni … Hakika yeye amechangia kwa malezi yake mema ya mtoto. Naye anao wengine pia, wahudumu waliooa pia, na hawa ni wainjilisti na wamo hudumani, na wengineo. Kwa hiyo ni jambo kuu tu.

8 Sijamwona Dada Palmer. Kweli, sijui kama ningemjua kama ningalimwona, ama la. Yeye yuko, labda,

mahali fulani (bila shaka) mkutanoni. Huko nyuma kabisa; Mungu akubariki, Dada Palmer.

Moyo wangu hutetemeka kila ninapowazia jambo hilo. Ndugu Palmer alikuwa tu amepanda vipandio ila dakika chache, mpaka nilipopata ujumbe kwamba alikuwa ameondoka. Sikuweza kuamini. Billy alinipigia simu, na mtu fulani alikuwa ameshika … nao walijua. Tulikuwa marafiki wazuri sana, na kujua ya kwamba alikuwa ameondoka, ilikuwa kweli inahuzunisha mno. Lakini sote hatuna budi kwenda, haidhuru sisi ni akina nani, hatuna budi kwenda mmoja baada ya mwingine. Ila kuna jambo moja tu, "Hebu na tusikie jumla ya maneno: Mche Mungu na uzishike amri Zake, kwa maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu," Mhubiri 12.

9 Sasa, sina wakati mwingi sana kwa ajili ya somo hili la shule ya Jumapili, nami nimepwelewa na sauti.

Aisee, Ndugu Pearry Green amefanya jambo zuri sana. Yeye alinisikia nikisema, jana usiku, "Nilikikosa kishungi changu kidogo cha nywele kunikinga …" Alipiga simu kule na kujaribu kumfanya mtu fulani anitumie kwa ndege. Nikasema, "Umechelewa sana, tayari nimepwelewa na sauti." Nilijaribu kwa miaka kadhaa kupata kisaidizi, bali wakati nilipokipata hicho, kilitibu jambo hilo. Lakini nilikisahau wakati huu, kwa hiyo kidogo nimepwelewa na sauti. Kwa hiyo mnivumilie, mkiweza, katika kunena.

10 Sasa, ni wangapi wanaopenda shule ya Jumapili? Loo, jamani, hiyo ni kweli. Ni jambo zuri kuwapeleka watoto wenu. La, hebu nisahihishe jambo hilo, jambo zuri kuwaleta watoto wenu. Hiyo ni kweli, kuwaleta watoto wenu; unakuja pia. Ni wangapi wanaojua namna shule yetu ya Jumapili ilivyoanzishwa kwa mara ya kwanza? Ilianzia wapi? Uingereza. Iliitwaje mara ya kwanza? *Shule matambara*. Hiyo ni kweli, inayoitwa "Shule ya matambara." Nimesahau jina la mtu huyo sasa aliyeianzisha. Jina lake lilikuwa nani? [Mtu fulani anasema, "Robert Raikes." — Mh.] Hiyo ni kweli, kweli kabisa. Naye aliwachukua maskini jamaa hao wadogo mtaani (walikuwa wamevaa matambara, wala hawakuwa na mahali pa kwenda, na wabaya sana), naye akawaleta na kuanza kuwapa masomo juu ya Biblia. Nayo imekua ikawa moja ya maagizo makuu sana ya kanisa, karibu, leo, shule ya Jumapili. Ni vizuri kwenda. Hakikisheni kuja, kuwaleta watoto wenu. Nafikiri maskani hapa yana waalimu, vyumba vyenye vifaa, umri, na kadhalika. Nanyi waongofu wapya mnaomjia Kristo, fuateni moja kwa moja kwenye Ujumbe; njoo hapa kwenye Maskani ya Uzima, nao watakufanyia mema.

11 Sasa, usiku wa leo tutakuwa na mstari wa maombi wa mtindo wa kale. Tutawaombea tu wagonjwa namna tulivyozoea, Ndugu Jack na Ndugu Brown.

Nakumbuka nilipomwona Ndugu Brown akijaribu kutoa hizo kadi za maombi, na jinsi yeye akiwa mhudumu mwenyewe, na katika siku hizo, katika madhehebu hilo lingekuwa, wao, wangemshinikiza, mnajua, "Mimi—mimi ni ndugu yenu. katika jambo hili," mnajua,"humna budi kuniweka juu hapa." Loo, hakika alikuwa na wakati mgumu, bali alidumu mwaminifu iwezekanavyo. Ndugu Brown ni mtu mmoja mzuri. Na kwa hiyo tunampenda.

12 Na ninapoona sisi sote, sisi watatu, tukifikia, tukiendea kwenye uzee, mwisho. Litakuwa ni jambo la kusikitisha sana kama hatungeweka ndani yetu jambo hilo kuu, kile tunachojua ni Kweli. Tunajitayarisha tu kurudi moja ya siku hizi, kurudi kwenye ujana wetu tena, kamwe … miili yetu imegeuzwa, ifanywe katika mfano Wake kusimama. "Kwa maana nyumba ya maskani yetu iliyo ya dunia hii ikiharibiwa, tunayo nyingine inayongojea."

13 Na sehemu yake yenye shukrani, rafiki mpendwa, ya kwamba Bwana Yesu mpendwa … Ninyi mnaoniamini kuwaambia Kweli; Bwana Yesu mpendwa, asubuhi moja yapata saa mbili, aliniruhusu kuiona Nchi hiyo. Sasa, haikuwa—haikuwa ni ono; bali sitaki kusema jambo hilo. Hata iwe nini, ilikuwa halisi tu kama ninavyonena nanyi hapa. Sasa, niliona nyuso za watu hao, nami sikuweza kuwatambua, walikuwa wamegeuka kuwa vijana tena. Nao walikuwa halisi kama … Ningewashika mikono yao na kadhalika. Halisi tu …

14 Nalo lilinisaidia, kwa kuwa nilikuwa na wazo: wakati mtu alipokufa, nafsi zao tu ziliondoka. Lakini wakati aliponinukulia hilo, ya kwamba "Kama nyumba ya maskani yetu iliyo ya dunia hii iki-…tunayo moja tayari." Mnaona? Nasi hatuna budi kuwa na kila kitu katika utatu, kufanya ukamilifu. Mnaona? Na kuna mwili mmoja hapa, halafu ule mwili pale ambao ule—ule mwili wa kimbinguni, halafu ule mwili uliotukuzwa katika ufufuo. Mnaona, hilo linaifanya iwe kamili. Mnaona? Kwa hiyo ni ninii … Si hadithi ya uongo, si wazo, si roho. Ni mwanamume na mwanamke kama ulivyo wewe, hasa kabisa.

15 Halafu basi, miaka mingi iliyopita, niliona maeneo ya waliopotea, na nilikuwa huko. Nakwambia, rafiki, kama mzee, hebu nikushawishie jambo hili, kote nchini asubuhi ya leo, kamwe usitake kupaangalia mahali hapo. Hakuna njia kamwe ambayo ningeninii…kama nilikuwa ni mwanasanaa akiwa na brashi nisingeweza kuchora picha hiyo. Kama mhudumu, nisingeweza kukuelezea. Nena kuhusu kuzimu kuwa ni mahali panapowaka moto, ni pabaya mara milioni moja kuliko huko, tishio linaloambatana nako.

16 Na Mbinguni … ama mahali hapa, popote pale, sijui nipaiteje. Yeye aliitaja pale kama "nafsi zilizo chini ya madhabahu." Lakini wakati palipokuwa, sijawahi … Hakuna njia ya kuelezea namna kulivyo kukuu. Kuna

… Sasa, inakubidi tu kuchukua neno langu, mimi ni mwanadamu tu. Mnaona? Lakini maono haya ambayo daima yametimia kama tu nilivyowaambia, nanyi mnajua kila moja limekuwa ni kweli, *hilo* ni kweli pia. Lolote mfanyalo, iwapo mtakosa kila kitu kingine (afya, nguvu, macho yako, chochote kile), msipakose Hapo. Hakuna kitu kinachoweza kulinganishwa napo. Ni … Hakuna—hakuna neno katika lugha ya Kiingereza, ninalojua, ambalo lingeweza kupaelezea. Kama ungesema "kamilifu," ni zaidi ya hilo, "shani," ni —ni zaidi ya hilo, "adhimu,"… Hakuna—hakuna maneno ambayo najua ambayo yangeweza kupaelezea, kwa sababu palikuwa ni … Na halafu, kuwazia, huo si mwisho wake bado. Nikawaza, "Mimi niogope kuja kwenye jambo hili?"

Nikasema, "Ninyi huwa mnakula?"

Kasema, "Siyo hapa. Hatuli hapa, bali tutakaporudi duniani tutaupokea mwili ambao unaweza kula."

17 Vema, ningeweza kuwahisi. Walikuwa hivyo tu. Mnaona? Nao … Nikasema, "Vema, una …" Loo, naam, wana mwili. Si kwamba ni hadithi tu, ni mwili. Tunafahamiana. Wote walinijua, walikuwa wakinikumbatia, mamilioni yao.

Nami nikasema, "Vema, ninataka kumwona Yeye aliyenileta hapa."

Akasema, "Huwezi kumwona sasa, huna budi kungojea."

Nikasema, "Kwa nini ukaniweka kwenye … hapa juu?"

Kasema, "Ulikuwa kiongozi maishani."

Nami nikasema, "Unamaanisha hao wote ni Wabranham?"

Akasema, "La! Hao ndio waongofu wako kwa Kristo." Mnaona?

18 Nikaangalia huku na huku, halafu basi siku hizo ngumu usiku, na majaribu, yakapita, wakati ningeweza kuziona nyuso zao. Msichana mmoja alikimbia pale, mmoja wa wanawake warembo sana, naye akanikumbatia tu kwa mikono yake, na kusema, "Ndugu wa thamani." Na wakati alipopita … Sasa, yeye alikuwa mwanamke. Kwa hiyo … Lakini mle ndani, hakutakuwako na dhambi kamwe. Mnaona, tezi zetu zimebadilishwa pale. Hawatawalea watoto tena, pale. Mnaona? Mnaona, yote ni sawa.

Kinacholeta tofauti, ni mhemuko. Hiyo ndiyo sababu siamini katika kucheza dansi. Hakuna mtu … Mimi, mbele za Mungu na Biblia yangu, nimeishi msafi, kama hivyo katika maisha yangu nilipokuwa mvulana mdogo, kote katika ujana wangu. Msichana yeyote niliyepata kwenda nje naye, ninaweza kwenda moja kwa moja Hukumuni pamoja naye. Mnaona? Lakini hakuna mwanamume, sijali wewe ni nani, anayeweza kumwacha mwanamke (katika umbo la mwanamke) akukumbatie kwa karibu; kama wewe ni mwanamume wa kweli mwenye afya, kuna mhemko. Lakini haukuwako pale; hamna tezi. Ninyi nyote mna tezi ile ile. Mnaona? Upendo tu safi, usioghoshiwa, wa ndugu, dada, zaidi ya vile ungekuwa kwa nanii wako…hata kwa nanii wako…kumkumbatia binti yako mdogo. Mnaona? Binti yako mwenyewe, hata hivyo amefanywa … yeye ni wa kike na wewe ni mwanamume. Mnaona, ingeumba kitu fulani; lakini Kule haiwezi, dhambi imekwisha, yote imekwisha. Mnaona? Halisi … Upendo halisi, mtakatifu.

19 Nami nikamwangalia mwanamke huyo. Kulikuwa na … ilionekana kama mamilioni yao pale, nao wote walikuwa na nywele ndefu, na nguo nyeupe. Na—na Huyu aliyekuwa akinena nami, akasema, "Hivi humtambui?"

Nikasema, "La."

Kasema, "Yeye alikuwa na umri wa miaka tisini ulipomwongoza kwa Kristo."

"Neema ya ajabu, namna sauti ilivyo tamu." Mnaona? Hakuna njia tu ya kuelezea ni nini. Chukuani tu neno langu kama mnaniamini. Hakikisheni mtaninii…teketezeni kila daraja la ulimwengu nyuma yenu.

20 Ninaamini kanisa linaanza kuusikia Ujumbe, na kuanza kuufahamu. Lakini, enyi marafiki, sikilizeni, hatuna budi kukaa katika Uwepo wa Mwana, hatuna budi kuivishwa. Yetu—imani yetu haijaiva. Kiakili tunausikia Ujumbe ambao Mungu ametupa, na kuona ishara ambazo ametuonyesha, na kuzithibitisha kwa Biblia, ziko, lakini, loo, namna ambavyo kanisa linapaswa kukaa Mbele Zake mpaka liwe jororo, mwajua, na liwe tamu katika Roho ili kwamba liweze kuoshwa. Wakati mwingine katika kuhubiri Ujumbe, unakuwa mkali, inakubidi kuuvunja namna hiyo, kwa sababu inakubidi kupigilia msumari kuufanya ushikilie. Lakini Kanisa likiisha kuupata, Wateule wanaitwa na kutengwa, kisha waingie kwenye Uwepo wa Mungu, najua itakuwa kitu kama watu walivyokuwa Pale wakati litakaponyakuliwa.

21 Nilikuwa nizungumze asubuhi ya leo juu ya Kunyakuliwa, bali sina sauti ya kutosha kufanya jambo hilo, na kwa hiyo mnivumilie tu kwa muda kidogo. Yale ninayotaka kuzungumzia, somo la: *Mahali Pekee Palipowekwa Na Mungu Pa Kuabudia.*

Sasa, ni somo kubwa mno. Kwa hiyo hebu na tuombe sasa. Na huko nje kote nchini asubuhi ya leo,

popote mlipo, inamisheni vichwa vyenu kwa dakika chache tu. Iweni waaminifu sana sasa, tunalikaribia Neno la Mungu, ambalo ni Mungu katika maandishi.

22 Mwandishi Mkuu wa Kitabu hiki, "Ni Mbegu," tunafundishwa, "ambayo mpanzi alipanda," ndivyo alivyosema Mwandishi. Sasa, tunatambua ya kwamba mbegu itakua kama iko katika ardhi nzuri. Kwa hiyo, Baba, je! Asubuhi ya leo utaondoa magugu yote na michongoma, na kutokuamini, na mawazo ya kushuku kutoka mioyoni mwetu; ili kwamba Neno la Mungu lipate kukua kwa uhuru, likiwa limetiwa maji na Roho mioyoni mwetu, tupate kuwa watu wa Mungu. Tujalie, Baba. Hiyo ni mioyo yetu. Si kwa sisi tu ambao tumetambua jambo hili, bali jalia kuwe na wengine kote nchini, kila mmoja moyo wake ukiwaka kwa upendo na wema, ataenda kujaribu kumpata ndugu aliyepotea, yule dada aliyepotea. Tujalie leo, Mungu. Tunakutazamia Wewe kabisa, kwa kuwa Wewe ni Kiongozi wetu na Bwana wetu. Kwa hiyo tunaomba ya kwamba utatuongoza katika Neno Lako leo, na utupe baraka Zako. Kwa neema Yako na katika Jina Lako tunaomba. Amina.

23 Sasa, hebu tuchukue somo letu … Ninataka kusoma kutoka katika Kitabu cha Kumbukumbu la Torati, Agano la Kale, kwa ajili tu ya Maandiko. Nina maandishi machache niliyoandika upesi baada ya kurudi kutoka kwenye kiamshakinywa pamoja na Ndugu Vayle.

Kamwe sikuweza kumshukuru yule mtu kwenye ile hoteli…ule mkahawa hivi majuzi usiku, aliyelipia chakula che—chetu cha jioni. Mimi na mke wangu pamoja na msichana wangu mdogo tulikuwa kule, na nilipoenda kulipa bili yangu, mtu fulani alikuwa ameilipa. Ye yote yule aliyekuwa, nakushukuru. Kasema, "Yule mtu aliyeketi mwishoni mwa benchi." Bila shaka kulikuwako na kundi zima mle ndani ambalo tulilijua. Sasa, mimi … namna fulani ya Kickapoo, kitu kama hicho, mahali hapa nje, mgahawa tuliokuwamo. Asante, ye yote yule aliyefanya hivyo. Kila mmoja wenu, Mungu awabariki.

24 Sasa, katika sura ya 16 ya Kumbukumbu la Torati, ni kuadhimisha pasaka. Kwa hiyo tunataka kusoma kuhusu vifungu vichache vya kwanza, vifungu vya kwanza vinne ama vitano, sita hapa.

> *Utunze mwezi wa Abibu, ukamfanyie pasaka ... (Hiyo inamaanisha "Aprili.") ... Bwana, Mungu wako, kwa kuwa ilikuwa ni mwezi wa Abibu alipokutoa Misri usiku Bwana; Mungu wako.*
>
> *Nawe umchinjie pasaka Bwana, Mungu wako, katika kundi la kondoo na la ng'ombe, mahali atakapochagua Bwana apakalishe jina lake ...*
>
> *Usimle pamoja na mikate iliyotiwa chachu; siku saba utakula naye mikate—mikate isiyotiwa chachu, nayo ni mikate ya mateso; kwa maana ... ulitoka nchi ya Misri kwa haraka; ili upate kukumbuka si... siku uliyotoka nchi ya Misri, siku zote za maisha yako.*
>
> *Wala isionekane kwako ... chachu muda wa siku saba katika mipaka yako yote; wala katika hiyo nyama uchinjayo siku ya kwanza jioni, kisilale cho chote usiku kucha hata asubuhi.*
>
> *Usimchinje pasaka ndani ya malango yako yote akupayo Bwana, Mungu wako;*
>
> *Ila mahali atakapochagua Bwana, Mungu wako, apakalishe jina lake, ndipo mtakapomchinja pasaka jioni, katika machweo ya jua, kwa wakati kama uliotoka Misri. Sasa Bwana na aongeze baraka Zake katika kusomwa kwa Neno Lake.*

25 Sasa, je, maikrofoni zina kasoro ndani yake? Jana usiku nilisikia walikuwa. Mnaweza kusikia vizuri, kote? Hamwezi kusikia. [Ndugu Branham anarekebisha maikrofoni — Mh.] Je, hilo ni bora zaidi? Je! Hii ni bora zaidi, tukizungumza na maikrofoni chini namna hii? Mimi kidogo nimepwelewa na sauti, kwa hiyo ninasimama karibu asubuhi ya leo kwa kusudi hilo, nami natumaini ya kwamba Ndugu Pearry anaweza—anaweza kulipata huko nje. Mnaweza kusikia vizuri sasa? Nafikiri wamelitengeneza. Vema.

26 Sasa, ile … Jambo ninalotaka kuzungumza juu yake asubuhi ya leo ni kwamba Mungu ana mahali pamoja tu ambapo mwabudu anaweza kukutana na Mungu, mahali pamoja tu. Katika nyakati zote wengi wametafuta mahali hapa pa siri pa Mungu, katika nyakati zote. Hata Ayubu alitaka kujua mahali alipoishi, "Laiti ningaliweza kwenda nyumbani Mwake na kupiga hodi mlangoni Pake." Ayubu alitaka kuona mahali anapoishi Mungu, maana hapo Mungu na familia Yake wanaabudiwa pamoja.

Kama vile jana, katika ule ujumbe jana asubuhi, tunaona ya kwamba kuna uwezekano wa mtu kumwabudu Mungu bure, kwa ibada ya uaminifu. Mungu ameyaandaa mambo hayo yote kwa ajili yetu, lakini jambo ni kwamba, inatupasa kutafuta tupate kujua mahali yalipo. Paulo alimwambia Timotheo kutafuta, na ku—kuwa katika wakati unaofaa na usiofaa, tayari kutoa ne—ne—neno ama…ya tumaini lililokuwa ndani yake.

27 Sasa, mambo haya yote yako mle ndani. Nasi tunaona … Wakati mmoja ningetaka kuja Shreveport ambapo tuna yapata tu majuma mawili ama matatu tu kuchukua tu dakika thelathini kila usiku na

kufundisha tu, mnaona, tukae tu moja kwa moja kwenye Neno, vifungu hivi vya siri, mnaona, ambapo tungeweza kupata tu kujua namna ya kuingia. Nanyi mwangalie tu, muufuate mwelekeo wa Mungu, kuna ufunguo mmoja tu kwa kila mlango. Hiyo ni kweli. Wala hakuna ufunguo mwingine, haidhuru unafananaje nao, Mungu hana ufunguo wa malaya; ana ufunguo mmoja tu. Na sasa, huna budi kuwa na ufunguo huo, la sivyo mlango hautafunguliwa. Haidhuru wewe ni mwaminifu jinsi gani, bado huwezi kufungua mlango huo.

28 Sasa, ni wangapi waliokuwa kwenye kiamshakinywa cha jana, asubuhi iliyopita? Vema, nafikiri karibu wote, angalau asilimia tisini yenu, ama zaidi. Kuwekea msingi jambo hili, yale nitakayosema, Daudi alikuwa mfalme aliyetiwa mafuta (aliyetiwa mafuta na Mungu), mfalme mkuu sana Israeli waliyepata kuwa naye, nje ya Bwana Yesu (ambaye ni Mungu) Mpakwa Mafuta. Daudi ni mwanawe, au, Yesu alikuwa Mwana wa Daudi kulingana na ukoo, mwili. Naye ataketi kwenye kiti cha enzi cha Daudi kama mtu atakayerithi, kama vile m—mwana wa mfalme daima anavyorithi kiti cha m—mfalme.

Angalieni, sasa, ya kwamba Daudi akiisha kutiwa mafuta, hata hivyo kwa upako alifanya, alitoka katika mapenzi ya Bwana akiwa na upako huo; na watu wote, bila kuchukua mwongozo wa Maandiko wala ufunguo wa ufunuo huu, wote wakiwa wametiwa mafuta pia, wote, pamoja, wakipiga kelele na kumsifu Mungu kwa jambo lililoonekana kuwa sawa kabisa: kulirudisha Neno la Mungu nyumba ya Mungu, kulirudisha Neno la Mungu kwenye nyumba ya Mungu. Lakini Daudi alikuwa mfalme, si nabii. Mnaona? Yeye … Kulikuwako na nabii nchini wa kufanyia jambo hilo, ndipo Mungu akadharau mwenendo huo wote kwa sababu kamwe hawakutumia ufunguo unaofaa. Mlango huo haukufunguka. Na sasa hatuna budi kukumbuka jambo hilo, na kuliweka hilo niani. Kuna … Kila kitu cha Mungu, njia moja fulani inavyopaswa kufanywa, na hiyo inatosha. Sasa, hapo Mungu ana Kanisa moja fulani ambalo Yeye hukutana na watu ndani yake, Naye atakupokea katika Kanisa hilo wala si kanisa lingine.

29 Nimesema jambo hili kwa sababu mara nyingi nimeeleweka vibaya, na watu wameniambia … Ninasema, "Je! Wewe ni Mkristo?"

"Mimi ni Mbatisti." "Je! Wewe ni Mkristo?"

"Mimi ni Mmethodisti."

"Je! Wewe ni Mkristo?"

"Mimi ni Mpentekoste."

Sasa, mnaona, hilo halimaanishi jambo moja kwa Mungu. Unaangaika tu na ufunguo usiofaa. Lakini kuna ufunguo sahihi, kuna mmoja ambapo Mungu … Mungu kamwe hakukuahidi kukutana nawe kama Mmethodisti, ama kama Mbaptisti, ama Mpentekoste, wala hakuna dhehebu lingine. Hata hafikirii madhehebu, yanampinga.

Kwenye Ujumbe huo mrefu, nitaupata maskanini hivi karibuni. Ndipo Ndugu Jack atausikia, ndipo mnaweza kuona kile mnachotaka kufanya nao, kwa kuwa utarekodiwa.

30 Sasa, watu hutenda kama Mungu anawajibika kukutana nao tu juu ya msingi wa theolojia yao. Sasa, watu hutenda hivyo. Hawatashirikiana hata mmoja kwa mwingine. Wa Utatu ama Pentekoste hawatashirikiana na wa Umoja, wala wa Umoja kushirikiana na wa Utatu. Mmethodisti hatashirikiana na Mbatisti, kwa sababu mmoja ni mshika sheria na mwingine Mkalvini, kwa hiyo hawana ushirika hata kidogo. Nao wanazivuruga nia za watu sana hata wanachukiana.

31 Nilienda kuomba, wakati fulani uliopita, katika chumba cha hospitali. Kulikuwa na mama aliyelala pale mgonjwa sana, akifanyiwa upasuaji, walimtarajia kufa. Bibi mwingine aliyelala pale (niliitwa kumwombea.), Nikamwambia, "Ungejali kwa muda kidogo tu nikiomba?"

Naye akasema, "Funga pazia hilo!"

Nami nikasema, "Samahani." Nikasema, "Nilikuwa tu ninataka kufanya maombi."

Akasema, "Funga pazia hilo!"

Nikasema, "Naam, mama." Yeye na mwanawe wameketi pale, anaonekana kama maskini Ricky wa kawaida. Nami nikasema, "Vema, wewe si Mkristo?"

Akasema, "Sisi ni Wamethodisti!"

Kasema, "Vema, sikukuuliza kamwe hilo, nilikuuliza kama ulikuwa 'Mkristo.'" Mnaona?

Na kwa hiyo akasema, "Funga pazia hilo!"

Mnaona, kwa kuwa mtu asiyekuwa Mmethodisti alikuwa akitaka kuomba dua kwa ajili ya mwanamke aliyekuwa akifa, huku naye pia yu anakufa. Lakini kwa sababu hakuhusika na dhehebu lake mwenyewe,

hata hakutaka kusikia hilo wala kuwa na uhusiano wowote nalo. Kama huyo si Farisayo, sijapata kumwona mmoja!

32 Ngojeni mpaka mtakaposikia *Mkondo Wa Nyoka*. A-ha. Vema. Sasa, wazia sasa ya kwamba madhehebu yao ndiyo pekee yanayosajiliwa na Mungu: "Mungu hatakusikia isipokuwa wewe ni Mmethodisti, ama Mbatisti, ama wa U—Utatu, ama wa Umoja," ama kitu kama hicho. Hilo ni kosa!

Na hilo ndilo kusudi langu; bali kama kuna sha—shauku katika nia na mioyo ya watu kuwa sawa … Siamini mwanamke huyo alifanya hivyo kwa sababu … ama mtu yeyote yule. Mmethodisti hatasimama na kulitetea kanisa la Kimethodisti kwa sababu a—alijua limekosea. Mtu huyo anafikiri ni sawa. Siamini wa Utatu angemhukumu wa Umoja, ama wa Umoja wa Utatu na Mpentekoste, kwa sababu anataka kuwa tofauti, anafikiri yeye yuko sawa. Mnajua, blanketi linaenea pande zote mbili. Lakini, kumbukeni, katika yote hayo, kama kuna jambo fulani ndani ya moyo wa mwanamume ama mwanamke ambalo waliamini ya kwamba hilo ni "kweli," basi inabidi pawepo na mahali fulani palipo sahihi. Kama nilivyosema mara nyingi, "Kilindi kinapoita kilindi, hapana budi pawe na kilindi cha kuitikia wito huo."

33 Mnajua, tumeambiwa ya kwamba—ya kwamba sili wakati mmoja alitembea kwenye ufuko wa—wa bahari, kwa miguu. Bali sasa hana miguu, iligeuka ikawa mbawa kwa sababu angeninii…alihitaji hizo mbawa wakati alipotoka nchi kavu, mnyama anayetoa manyoya, akahamia baharini; maumbile yalimtengenezea mbawa badala ya miguu, maana angeweza kuelea zaidi ya alivyotembea.

Siwezi kumkumbuka mtu huyu mashuhuri aliyeenda kwenye Ncha ya Kusini. Jina lake lilikuwa nani? Byrd Wanasema ya kwamba aliwatengenezea ng'ombe makoti, kwenye ziara hii ya uvumbuzi; ambako alikuwa amewapeleka ng'ombe kwa ajili ya maziwa. Naye akawatengenezea makoti ya manyoya kuwakinga ng'ombe wasife kwa baridi. Lakini alipofika kule, hawakuhitaji koti lolote la manyoya, maumbile yalikuwa yamewakuzia moja. Mnaona? Kwa nini? Kabla hapajakuwa na pezi mgongoni mwa samaki, ilibidi pawe na maji apate kuogelea mle la sivyo kamwe asingekuwa na pezi. Kuna … Kabla hakujakuwako na mti wa kukua duniani, ilibidi kuwe na ardhi kwanza kukua ndani yake, la sivyo hakungekuwa na mti.

Kwa hiyo, mnaona, mradi tu kuna kitu fulani katika moyo wa mwanadamu kinachohitaji kitu fulani, hapana budi kuwe na kitu fulani huko nje cha kuitikia, kuridhisha mwito huo.

34 Mwanamke … Uchunguzi wa maiti ulifanyika hapa muda fulani uliopita juu ya mwanamke aliyekufa. Na sababu, wao—wao wanadai, kilichomwua, yeye alikula vitunguu mara kwa mara, wakati wote. Kama hakuwa akila vitunguu, kichwa chake kingekuwa kikiwasha, na kila kitu; wasingeweza kulitatua. Kwa hiyo walipofanya uchunguzi, walipata kivimbe katika mwanamke huyo cha namna fulani ya seli; walizipa ji—jina. Nao wangekichukua kivimbe hicho na kukiweka kwenye bakuli ya vitunguu, nacho kikaviyeyusha vitunguu hivyo usiku kucha. Mnaona? Ilikuwa ni kitu gani? Kilikuwa ni kitu fulani ndani ya mwanamke huyu kikililia vitunguu, na kama kusingalikuwa na vitunguu kusingalikuwa na uvimbe.

Kwa maneno mengine, hapana budi kuwe na Muumba kwanza, kabla hakujakuwako na kiumbe. Mnaona?

35 Sasa, kama katika moyo wa mwanadamu kuna shauku Sasa, kama katika moyo wa mwanadamu kuna shauku, kama vile Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Katoliki, hawa wote wengine, wakijaribu kupata hiyo njia moja ya kweli, nao wanaambiwa na makasisi wao na wachungaji, na kadhalika, ya kwamba "Hii ndiyo njia ya kweli." Wanasema, kasisi anasema, "Hakuna wokovu nje ya kanisa Katoliki."

Vema, kila kanisa huchukua ninii yake … wazo lao wenyewe. Wengine wao hawatakubali jambo hilo, bali wanafanya hivyo kwa matendo yao. Matendo yako yananena kwa sauti kubwa kuliko neno lako. Ni ninii tu … Kwa njia nyingine, wao ni wanafiki zaidi kuliko Wakatoliki walivyo. Wakatoliki wanakiri hilo moja kwa moja, "Ninaamini ya kwamba hili ndilo jambo pekee," bali hawatafanya jambo hilo. Wanalificha, lakini matendo yao yanathibitisha yale wanayowazia. Mnaona?

36 Sasa, hapana budi pawe na mahali pamoja, kwa sababu kuna shauku katika moyo wa mwanadamu kuipata. Nami nafikiri ya kwamba Neno la Mungu lina jibu kwa kila kitu tunachohitaji. Kwa hiyo Mungu ana jibu, na hebu tulitafute sasa katika Maandiko. Na basi kama Mungu atatuonyesha kwa Maandiko mahali pekee, eneno pekee (dhehebu pekee, kama ndivyo ilivyo), njia pekee ambayo Mungu atakutana na mwanadamu, basi tunapaswa kushikilia jambo hilo kwa sababu tumepata Kweli ya Biblia, kile inachosema.

37 Sasa, neno *Kumbukumbu la Torati*, neno lenyewe linamaanisha "sheria mbili," *neno Kumbukumbu la Torati*. Na Mungu ana sheria mbili. Zile sheria mbili: moja ya hizo ni kutotii Neno, na ufe; na hiyo nyingine ni kutii Neno, upate kuishi. Hizo ndizo sheria mbili, na Kumbukumbu la Torati maana yake ni hizo sheria mbili. Zote mbili zimewekwa wazi kwetu kikamilifu katika Maandiko. Moja ya hizo ni mauti, hiyo nyingine ni Uzima; Uzima na mauti. Mungu hutenda kazi tu katika Uzima, Shetani katika mauti tu. Na haya yalionyeshwa kwa ulimwengu hadharani, wazi mbele ya kila jicho, na hakuna udhuru kwetu. Moja ya hizi ilikuwa, ilionyeshwa juu ya Mlima Sinai wakati torati ilipotolewa, ambayo iliihukumia kifo jamii yote ya binadamu; hiyo nyingine ilitolewa juu ya Mlima Kalvari, ambayo iliipa jamii yote ya binadamu Uzima, hapo

adhabu ilipolipiwa katika Yesu Kristo. Hizo sheria mbili za Kumbukumbu la Torati zilitimizwa katika mambo haya mawili makuu.

38 Ninawatakeni mwone tena, kulikuwako pia na maagano mawili yaliyotolewa. Agano moja lilitolewa kwa Adamu, ambalo lilikuwa kwa masharti, kama sheria: "*Usipogusa* hiki, basi utaishi; bali ukigusa hiki, utakufa." Hiyo ilikuwa ni sheria. Halafu kulikuwa na sheria nyingine aliyopewa Ibrahimu, ambayo ilikuwa kwa neema, bila masharti: "Nimekuokoa wewe na uzao wako baada yako." Amina! Huo ni mfano wa Kalvari, si mfano wa—wa—wa agano la Adamu, ni agano la Ibrahimu.

Lakini sasa tunamsikia akisema kuna mahali pamoja tu ambapo atakutana na mwanadamu kuabudu. Tunalisoma papa hapa katika fungu la maneno. Tutairejea, huko nyuma, katika dakika chache.

39 Basi kama kuna mahali pamoja tu ambapo Mungu hukutana na mwanadamu, afadhali tuwe waangalifu sana. Sasa hebu na tuweke kando mapokeo yetu asubuhi ya leo, na … katika somo hili la shule ya Jumapili, na tuwe na hakika sana ya kwamba tunapata mahali pamoja. Kwa sababu, Mungu amesema hapa, Yeye hatakupokea mahali pengine popote. Kanisa lingine lo lote, Yeye hatakupokea. Ni katika Kanisa Lake tu, ndipo mahali pekee atakapokupokea.

Sasa, "Unasema nini, Ndugu Branham? Kama mimi ni mwaminifu?" La.

Kumbukeni, Yesu alizungumza na watu fulani waaminifu, waabudu wa siku Zake, Naye akasema, "Mwaniabudu bure." Ibada ya kweli, ya kweli kutoka kilindi cha mioyo yao. "Mnaniabudu bure, mkifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya mwanadamu," ama kanuni zao za kimadhehebu. Waaminifu, wenye uchaji, wa kidini wawezavyo kuwa. Na hilo halikuwa geni kwa Mafarisayo. Kaini na Habili, wale waabudu wawili wa kwanza waliozaliwa, kuzaliwa kwa kawaida hapa duniani, walikuja kabisa katika mtazamo ule ule.

40 Kaini alikuwa wa kidini tu kama Habili alivyokuwa. Wote wawili walijenga madhabahu. Wote wawili walimpenda Mungu. Wote wawili walitoa dhabihu. Wote wawili waliabudu. Wote wawili walitoa fungu la kumi. Wote wawili walifanya kila kitu sawa tu. Lakini Habili, kwa imani ambayo ni "ufunuo," Neno la Mungu lililofunuliwa, kufanywa dhahiri, kudhihirishwa, na kuthibitishwa. Utukufu! Kaini alitoa sadaka, bali Mungu hakuithibitisha. Mungu alihitaji kuabudiwa, na Kaini akatoa sadaka, bali Mungu hakuithibitisha. Lakini kwa njia ya kweli …

Unasema, "Vema, kanisa langu Ndilo. Jamani …"

Ngoja kidogo. Mungu hulifasiri Neno Lake Mwenyewe kwa masharti Yake aliyonena. Mnaona, Kaini alisema, "Mimi ni wa kidini. Mimi ninampenda Muumba wangu. Ninakutolea Madhabahu hii nzuri. Ninakutolea sadaka hii. Nilijenga mambo haya yote, Bwana, kwa sababu ninakupenda." Habili alisema jambo lile lile. Sasa ni ile iliyothibitishwa, ile iliyohakikishwa. Ndipo Mungu akashuka na kupokea dhabihu ya Habili, kwa sababu kwa ufunuo alikuwa ameshika njia ya kweli ya Mungu iliyokubalika.

41 Sasa angalia hiyo roho ya Kaini ikishuka moja kwa moja kupitia Maandiko, moja kwa moja hadi kwenye siku hii ya mwisho kabisa. Kimsingi? Kimsingi tu kama hicho kingine kilivyokuwa.

Mwangalie nabii Balaamu na nabii Musa. Wote wawili wakiwa na madhabahu saba, madhabahu ya Yehova, damu juu ya kila moja; wala si hayo tu, bali kondoo dume juu ya kila moja. Katika tarakimu, ni hesabu sahihi kabisa, saba, "kamilifu," kondoo dume saba. Ni sawa kabisa, madhabahu zote mbili. Likiwa la kimsingi kama moja lilivyokuwa, hilo lingine pia. Lakini Mungu alimthibitisha nani? Mnaona? Mnaona? Yule aliyekuwa katika Neno Lake. Kimsingi halina maana sana; ni ufunuo wa Mungu.

42 Sasa wazia! Watu hawa, kwa nini waliitwa na kuwekwa katika hali hii (Mafarisayo hawa) na Yesu, kasema, "Mnaniabudu bure"? Mwabudu Yeye: ibada halisii, ibada ya kweli kutoka mioyoni mwao. "Wewe … Mnaniabudu bure." Kwa nini? Wakifundisha mafundisho yaliyo mapokeo ya wanadamu. "Kwa hiyo mnazitangua amri za Mungu kwa watu."

Kama ningewafundisha ujumbe wa Kimethodisti, haungewafaa, huu ni wakati wa Bibi-arusi. Kama Musa angefundisha ujumbe wa Nuhu, haungefaa kitu. Kama Yesu alifundisha ujumbe wa Musa, haungefaa kitu. Kwa sababu mbegu zilizochaguliwa tangu zamani zimekaa pale ambazo zitatiwa maji tu na aina hiyo ya maji yanayotolewa kwa mbegu hiyo. Mnaona? Haitachipuka kwa mazingira mengine yoyote. Hayana budi kuwa ni mazingira yanayoichepusha.

43 Sasa, unaweza kuchukua yai la kuku na kuliweka kwenye kiangulio, ambacho kinapaswa kuwa chini ya kuku, bali litaanguliwa kwa vyovyote vile. Ukiliweka chini ya kitoto cha mbwa litaanguliwa. Ni joto, hali inayolifanya lianguke. Kwa hiyo halina budi kuwa chini ya masharti. Ungeweza kuchukua yai zuri lililo hai na kuliweka chini ya kuku aliyekufa, halitaanguliwa. Mnaona? Mnaona, ni hali yake.

Vema, hivyo ndivyo ilivyo katika wakati huu tunaoishi, huna budi kutafuta njia ya Mungu ya kufanya jambo hilo kwa wakati huu. Hiyo ndiyo Martin Luther aliyopata, hiyo ndiyo John Wesley aliyopata, hiyo ndiyo Wapentekoste waliyopata katika wakati wao. Wakati wa Mungu na wakati wa kufanya jambo hilo.

44 Sasa, Wapentekoste. Huyo ndugu, mmoja … Ninaamini ninii … jicho lake moja lilikuwa limetoka, ndugu mweusi ambaye kweli alianzisha ujumbe wa Kipentekoste huko California, ule mtaa wa kale wa Azusa. Alichekwa, kwa sababu alikuwa ni mnegro. Alidhihakiwa, bali alileta ujumbe kwa ajili ya wakati huo. Mwili mdogo tu, ilikuwa vigumu kwa jamaa kuandika jina lake mwenyewe, bali Bwana alikuwa amemfunulia ya kwamba huu ulikuwa ndio wakati wa kurudishwa kwa karama hizo, nao wakaja. Haidhuru ni *yapi* yaliyosemwa, vipawa vilikuja. Lakini kila mtu aliingia kwenye mazingira yake, na akaona ilikuwa ni wakati huo, na akaona Mungu akithibitisha ya kwamba hao watu wangeweza kunena kwa lugha, na kadhalika, ilitukia. Lakini wakati alienda na kushikilia ya kwamba "huu ndio ushuhuda wa pekee," hiyo ililiua. Mnaona? Linaendelea tu moja kwa moja, mnaona. Hiyo ilifanya hivyo. Ndipo wakaanza kutenganisha *hiki, kile*, na kuunda madhehebu; na mmoja ati atakuja kwa wingu, na mwingine anakuja katika kichaka. Na loo, jamani, hilo hapo linaenda.

45 Hivyo ndivyo madhehebu yanavyofanya. Mnaona? Mungu si mwanzilishi wa madhehebu, kwa sababu madhehebu ni Babeli, na Yeye si mwanzilishi wa mchafuko. Tunaona ninii yake yote … Haikubidi kuwa hata msomi kuona hilo. Ni Babeli! Mnaona? Mapokeo (wazia jambo hilo), watu wanyofu. Sasa, bado, kwa sababu wanaamini jambo hilo, bado kuna haja ya kuwa na mahali pamoja paaminifu ambapo Mungu hukutana.

Sasa angalia kifungu cha 2. "Kuabudu mahali ambapo nimechagua." Ile sadaka, hakika, ambapo waliabudia juu ya sadaka. "Mahali nilipopachagua; si kile ulichochagua, kile mwanadamu alichochagua. Lakini kile nilichochagua, mtaabudu mahali hapa." Inaonyesha basi kuna mahali pamoja tu, pengine ni bure. Haipaswi kuwa ni chaguo lako, bali lazima liwe chaguo Lake.

"Vema, si lazima niende kanisani." Ama, "Wewe una mawazo finyu sana! Mbona, hata utawakemea wanawake kuhusu kuhubiri, na…ama kuhusu wanawake kukata nywele zao, na wanaume kuhusu mambo haya mengine. Mbona, wewe una mawazo finyu!"

Vema, haikubidi kuchukua njia ya Mungu kuhusu jambo hilo, unaenda mahali wanapofanya jambo hilo. Mnaona? Nawe utaona kwamba liko katika Maandiko, kwa hiyo, "Wananiabudu bure." Yesu alinena juu ya jambo lile lile. Mnaona?

46 Ili kwamba kila nukta ndogo, kila kitu, yakupasa uwe mwaminifu ndani yake. Daima ni mdogo—mzabibu mdogo, mdogo—maskini mbweha mdogo anayeuharibu mzabibu. Wakati mwingine unaacha … Si yale mambo makubwa unayofanya, ni yale mambo madogo unayoyaacha. Kumbuka, mnyororo una nguvu nyingi zaidi tu kwenye kiungo chake kilicho dhaifu kuliko vyote. "Heri wale wanaotii amri zote za Mungu, wapate kuwa na haki ya kuingia ndani." Fanya yote Mungu aliyosema.

Kama lilisema wanawake wawe na nywele ndefu, unasema … mwanamume mmoja aliniambia si muda mrefu uliopita, kasema, "Mimi sihubiri dini ya utakatifu wa mambo ya kuonekana kwa nje."

Nikasema, "Basi huihubiri Injili." Naam.

Mungu aliiweka pale, Yeye alisema la kufanya. Nawe ama unafanya hivyo … Hilo ni jambo lako la kawaida, la busara. Kitu kilicho kidogo…ninii…kitu kidogo kisicho na maana. Yesu alisema, "Heri wale ambao wangechukua kitu kidogo, wangefanya mambo madogo." Na mwanamke kuachilia nywele zake zikue, hiyo ni ninii tu…mbona, ni jambo ambalo yeye anaweza kufanya, wala hata hatafanya hilo. Hata hatafanya hivyo.

"Loo, tufundishe mambo makuu."

Unawezaje kufundisha mambo makuu, wakati hutafanya jambo rahisi, la kawaida? Kwa sababu, unaona, nia yako na kusudi lako ni baya.

47 Ni upendo wako kwa Mungu, "Bwana, sijali kile unachotaka nifanye, niko tayari kufanya hivyo." Ndipo unafikia mahali fulani, bali kama hulifanyi namna hiyo, namna alivyosema ulifanye…

Ni chagua Lake, "Mahali ambapo nimechagua." Hapo ndipo unapoabudu kwa dhabihu yako.

Unaweka … Kaini alileta dhabihu yake, Habili akaleta yake, inategemea unaipeleka mahali gani. Kama ukipeleka mahali ambapo Yeye amepachagua, itakuwa sawa, Yeye atakubali; Kama sivyo, Yeye hatakubali. Sijali, ni dhabihu ile ile, chochote ilicho, ingali hai-…inakataliwa, isipokuwa iletwe mahali hapo pamoja.

Sasa tunataka kuona ni wapi tunataka kuleta dhabihu hii. Tungeweza kujua … Sote tunataka kwenda Mbinguni. Sivyo? Nasi sote tunajua tumekosea. Sote tunaamini ya kwamba Yesu ndiye Dhabihu. Sasa tunataka kujua mahali pa kumpeleka, itakuwa—itakubaliwa. Mnaona? Hiyo ni kweli. Biblia inatwambia mahali pa kuipeleka, mnaona, nayo itakubalika; nje ya hapo, haitakubalika.

48 Hebu na tuone hapa pia mahali ambapo Yeye alichagua kwa ajili ya dhabihu kuwekwa, mahali ambapo Yeye alichagua kuweka dhabihu. Huwezi kuiweka kwenye yoyote ya malango haya; bali mahali

alipopachagua kuiweka, Yeye pia aliweka Jina Lake mahali hapo. Hivyo ndivyo alivyosema hapa. Yeye alichagua kuweka Jina Lake ndani yake. Sasa hebu na tuyachunguze Maandiko kwa ajili ya mahali hapa, kwa kuwa hapo ndipo mahali alipoliweka Jina Lake.

Sasa hebu na tusome kutoka kwenye fungu hili. Nami nilikuwa na kijikaratasi kidogo hapa ambacho mimi … asubuhi ya leo, kilinijia. Hebu na tuchukue kifungu cha 2 cha sura hii. Sasa, sitaki kushikilia kwa muda mrefu mno, kwa ajili ya watu, kwenye mitandao hii hapa nje. Sasa aya ya 2 ya sura hii ya 16:

> *Nawe umchinjie pasaka BWANA, Mungu wako, katika kundi la kondoo na la ng'ombe, mahali atakapochagua BWANA apakalishe jina lake.*

49 Sasa, huwezi kuchukua hili…uaminifu wako na yote unayotaka kukiri, kamwe huwezi kuyapeleka kwa madhabahu ya Methodisti, kwa madhabahu ya Baptisti, kwa madhabahu ya Pentekoste, bali kuna madhabahu mahali fulani alipopachagua ambapo Yeye…alikalishe Jina Lake mle, Naye angekutana nawe mahali hapo. Sasa, kama ukifanya kila kitu kiendelee vizuri, kitaendelea; kila kitu kimewekwa katika utaratibu. Kama kuna shoti kwenye waya huo, hiyo taa haitawaka; kwa sababu umekatizwa. Na wakati utalichukua moja la Maneno ya Mungu ama moja ya mahali Pake, na moyoni mwako mwenyewe uwe na malengo ya kichoyo, yatakatiza nguvu za Mungu papo hapo. Kama ukifanya hivyo kwa sababu unataka kuwa mjanja, unataka kuwa tofauti na mtu mwingine, ama chochote kile, papo hapo inakatika, itayeyusha fyuzi. Umekosea. Huna budi kuja na uaminifu, kwa moyo wako wote, nia zako na malengo yako yamewekwa moja kwa moja kwa Mungu. Halafu tafuta mahali *Pake*, tafuta mahali aliposema, na ulete pale. Mnaona?

50 Waangalie Martha na Mariamu. Wakati Yesu aliporudi, baada ya kuwafundisha Injili hii (Nuru ya siku Yake, Yeye akiwa Masihi), Yeye alichukiwa, akakataliwa. Loo, Mafarisayo na makanisa walimdharau. Lakini Lazaro alikuwa amekufa, yule ndugu aliyekuwa rafiki yake msiri. Yeye alimruhusu akae pale; nao wakamtuma, Yeye hata hakuja.

Lakini mwangalie Martha, mtazamo wake. Akasema, "Bwana, kama ungalikuwa hapa." Mpe hatimiliki Yake ya haki: Bwana, herufi kubwa B-W-A-N-A, Yahwe, Yehova. Utukufu! "Kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa." Uzima na mauti haviwezi kushirikiana katika njia ile ile, au nyumba ile ile. "Unge … Asingekufa."

Yesu alimwambia, "Mimi ndimi ufufuo na Uzima," asema Mungu. Mnaona? Wakati aliposema, kwanza, "Ndugu yako ataishi tena."

Akasema, "Naam, Bwana, kweli ninaamini jambo hilo. Kama mwanamke Myahudi, ninaamini kutakuwako na ufufuo wa wote waliokufa; nami ninaamini ya kwamba ndugu yangu alikuwa mwaminifu na mkweli katika ibada. Nami ninaamini ya kwamba Wewe Ndiye yule Masihi, aliyetajwa katika Biblia, kwa sababu Mungu akithibitisha Neno Lake ndani Yako inaonyesha ya kwamba Wewe Ndiye Mjumbe wa wakati huu. Wewe ni yule Masihi. Ninaamini ya kwamba Wewe ndiwe yule Kristo aliyekuwa aje, kwa sababu kazi Zako zinashuhudia ya kwamba Mungu amekutuma hapa kuwa Masihi huyo." Loo, jamani! Angalia gia zikiingia mahali pake sasa. Mnaona?

51 Sasa, yeye alikuwa na haki ya kusema, "Kwa nini hukuja na kumfufua ndugu yangu? Kwa nini hukumponya? Uliwaponya wengine. Rafiki yako wa karibu sana, na sasa angalia kilichotukia." La, la, nia ya namna hiyo haifiki po pote.

"Ninaamini ya kwamba Wewe ndiwe hasa unayetambulishwa kuwa katika Maandiko. Ninaamini hii ndiyo siku ambayo Masihi anapaswa kuja; tumekuwa tukiitazamia. Sijali hao wengine wanasema nini. Ninaamini kwa moyo wangu wote, kwa yale niliyoona na kusikia kwa Neno, ya kwamba Neno limethibitishwa ndani Yako, ya kwamba Wewe ndiwe yule Masihi." Mnaona, huko chini kabisa ndani yake, a—alikuwa anataka kuomba kitu fulani, bali ilimbidi kupitia njia ifaayo.

52 Vipi kama angalikimbilia pale na kusema, "Na basi unaniambia Wewe ni yule Masihi! Wala hata huna heshima, uungwana wa kutosha hata kuyajibu maombi yetu; wakati sisi tulikulisha na kukupa makazi, na kila kitu, na kukutetea, na kuyaacha makanisa yetu, kama vile ulivyotuamuru tutoke kwenye madhehebu hayo." Mnaona? "Na tumeyaacha, na sasa tunahesabiwa kama waasi na mahaini. Na kila kitu tulichokufanyia, halafu hata huna heshima ya kawaida ya kujibu wito wangu?" Sasa, kwa kweli, yeye alikuwa na haki hiyo.

Kama vile unavyosema kuhusu nywele zako fupi, "Mimi ni raia wa Marekani. Ninaweza kuvaa kaptura, kufanya chochote ninachotaka kufanya, si haramu." Hizo ni haki zako, bali kondoo daima hupoteza haki zake. A-ha. Kama wewe ni mwana-kondoo! Yeye hana kitu ila sufu, anapoteza hicho. Hizo ni haki zake alizopewa na Mungu, bali anaipoteza.

53 "Nina haki ya kujiunga na dhehebu lolote." Hiyo ni kweli kabisa, bali wewe unaipoteza hiyo. Mnaona?

Alipoteza yote aliyokuwa na haki nayo, kutambua Neno la Mungu lililodhihirishwa papo hapo mbele

zake.

Yeye alisema, "Mimi ndimi ufufuo na Uzima. Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi. Kila aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe. Unaamini jambo hili?" Mnaona, kulikuwako na kipengele kimoja zaidi ambacho hakuwa amekifikia. Mnaona?

"Naam, Bwana! Ninaamini ya kwamba Wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai!" Ee ndugu, kila kitu kilikuwa tayari kuanza papo hapo. Mnaona?

"Mmemweka wapi?" Mnaona? Nanyi mnajua kilichotukia.

54 Mnaona, huna budi kuingia mahali hapo panapofaa kabla Yeye hajapokea dhabihu yako. Mnaona, haina budi kuingia ndani yake. Sasa, tazama.

> *… Mahali atakapochagua BWANA apakalishe jina lake.*
>
> Usimle na *mikate iliyotiwa chachu;…*

Hiyo inaashiria nini katika dhabihu? Usiichanganye na kanuni yoyote ya imani, haina budi kuwa ni Neno. *"Pasiwepo na mikate iliyotiwa chachu."* Chachu ni ninii … Unajua chachu ni nini katika chochote. "Chachu kidogo huchachusha donge zima," donge zima ni ule Mwili. Huwezi kuweka chembe moja ya madhehebu ama kanuni ya imani katika Kristo. La, bwana, haitafaa kitu.

Mnakumbuka ujumbe wa Alhamisi iliyopita? Mume wako mzee lazima awe amekufa. Hiyo ni kweli. Mume wako mpya ni Neno.

> *…siku saba utakula naye mikate isiyotiwa chachu…*

"Siku saba," hiyo inaashiria nini? Zile Nyakati Saba kamili za Kanisa, siku saba. Kwa nini iliwabidi kula siku saba? Kabla ya nini? Kabla ya kutoka. Na wakati wote wa kanisa, tangu mwanzo hata mwisho, hauna budi kuishi tu kwa Neno la Mungu la wakati huo. Kwa hiyo kanuni yako ya imani ya Kirumi, Methodisti, Baptisti, na Pentekoste zote zimekufa.

55 Sasa angalia.

> … Ndani yake, *nayo ni mikate ya mateso; … Kuteswa kwa ajili Yake; Luther, Wesley, Wapentekoste; wote wakiteswa, na wewe pia utateswa.*
>
> *... kwa maana ulitoka nchi ya Misri kwa haraka; ili upate ... kukumbuka siku uliyotoka nchi ya Misri, siku zote za maisha yako.*
>
> *Wala isionekane katika…kwako chachu muda wa siku saba katika mipaka yako yote;…*

Katika yule Bibi-arusi mzuri wa Kristo, baada ya kuuawa kwake na Falme ya Kirumi kote kwenye zile Nyakati za Giza, kwamba ilimbidi Yeye kufa, "Punje ya ngano isipoanguka ardhini." Ilibidi Bwana arusi aje, Kipeo kikamilifu cha Mungu. Nyote mlisikia ujumbe wangu juu ya jambo hilo.

56 Nilisimama kule, Los Angeles, huko Forest Lawn, siku moja, na moyo wangu ukaruka. Ni wangapi waliowahi kuwa katika Forest Lawn? Kuna ninii … sanamu ya Musa na—na … -angelo, naamini ni, Michelangelo. Na ni sanamu kamilifu, yote ila kwenye goti la kulia; kuna mkato wenye kina cha kama nusu inchi. Naye yule kiongozi … Nilikuwa nikiangalia, naye akanionyesha. Yeye alisema, "Michelangelo alikuwa ametumia maisha yake yote kujaribu ku—kufanya … Yeye alikuwa mchonga sanamu, naye alikuwa akijaribu kutengeneza sanamu ya Musa. Nyuma katika nia yake, alikuwa anawazia sura ya Musa anavyopaswa kuwa. Alikuwa na hayo moyoni mwake, namna Musa alivyopaswa kuonekana. Ndipo akayatumia maisha yake yote; akichimba kidogo hapa kwa patasi, na kuisugua, anarudi nyuma na kuiangalia. Mwaka baada ya mwaka baada ya mwaka, aliifanyia kazi. Hatimaye wakati ilipokamilika, naye akarudi nyuma kidogo na kuweka chini kitambara chake na nyundo yake, aliiangalia ile sanamu. Ilifanana kamilifu sana na sura ya Musa aliyokuwa nayo moyoni mwake, hata akajisahau kabisa, akainyakua ile nyundo na kuipiga, akapaza sauti, 'Nena!'" Kinaitwa *Kipeo cha Michelangelo.* Hicho kitu fulani kikuu kwenye sanamu hiyo, lile ono alilokuwa nalo la yale Musa anayopaswa kuwa nayo, lilikuwa tu likionyesha mfano wa yule Baba Mungu mkuu.

57 Yeye alikusudia moyoni Mwake, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kuwa na Mwana, kwa kuwa Yeye ni Baba. Bali bado ilikuwa katika jeni za Neno Lake. Naye akamwumba mtu, na ilimbidi kumweka katika uhuru wa kuchagua, bali mtu huyo alianguka. Lakini yule Mchongaji mkuu, Mungu, aliyemfanya mwanadamu kutoka kwenye mavumbi ya ardhi, Yeye hakuridhika na jambo hilo, alianza kumfanya mwanadamu tena. Naye akamfanya Nuhu, akafa akiwa mlevi. Yeye alimfanya Musa aliyeshindwa kutimiza Neno Lake. Yeye aliwafanya manabii waliokimbia katika wakati wa shida. Naye aliendelea kujenga na kufinyanga mpaka baada ya kitambo kidogo alitaka ki—kipeo, kumwonyesha Yeye, tabia Yake, kile kilichokuwa moyoni Mwake namna mwana anavyopaswa kuwa.

58 Siku moja, huko chini Yordani, baada ya kile Kipeo kufinyangwa na kufanywa, huyu hapa akishuka chini katika…juu ya mbawa za Hua, kasema, "Huyu Ndiye!" Yeye alivutiwa sana na Kipeo hiki hata akampiga pale Kalvari, kwamba angelikufa kwa ajili yetu sisi wengine ambao si wakamilifu; ili kwamba kwa kumwaga Damu Yake, apate kuleta vipeo vingi (wakiwa ni Bibi-arusi) kwa Mwanawe. Kipeo kina kovu kwa sababu ya shauku ya Mungu kuona Kipeo kama hicho, Yeye alimpiga kwa ajili ya sisi sote. Mnaona? Hapo Yeye alikufa, kutukamilisha sisi ambao si wakamilifu. Kile Kipeo.

59 Angalia, hapa ndani Yeye alisema:

*… Siku saba utakula mkate huu usiotiwa chachu …*

Sasa, mkate ni mfano. Yesu alisema, "Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno." Si tu—Neno moja tu hapa na pale kama vile madhehebu yangewafanya mliamini. Lakini Neno la Mungu ni kamilifu! Ni Mungu Mwenyewe katika herufi, inayoitwa "Mbegu." Na imani ya kweli isiyoghoshiwa katika Neno hilo litaifanya hiyo Mbegu iwe Hai.

Hayo ndiyo mnayoona hasa usiku katika utambuzi, na mambo haya mengine yote, kwa maana ni ahadi ambayo Mungu alifanya. Naye alisimama karibu nami na kuniambia hivyo, na kuniambia hawa "waigaji watainuka, bali simama imara." Ninaamini jambo Hilo. Na hamna nia ya kichoyo, kumwudhi mtu yeyote, bali kuwa na kicho kwa Mungu na kufanya kazi aliyoniitia kufanya, hiyo ndiyo sababu ninasema mambo haya. Naye Mungu anayathibitisha, na kupokea matoleo na dhabihu, kwa kuyathibitisha kwamba ni Kweli. Hakuna swali Kwake! Sasa angalia Neno hilo!

60 Sasa, tunaona hapa, *"Siku saba,"* hiyo ni kwa ajili ya kila wakati wa kanisa. Sasa, ilibidi yule Kipeo afe, kusudi apate kufufuka na kutukomboa sisi sote. Ndipo akaweka kanisa katika Pentekoste, bali Kanisa hilo ilibidi lipitie dhabihu; na ulimwengu wa Kirumi uliuua, ukauweka ardhini.

Kama vile huyu mwandishi wa kitabu hiki, siwezi kukikumbuka sasa, alivyonidhihaki sana, na kusema, "Katika pepo wote, ni William Branham." Mnaona, hivyo ndivyo ibilisi anavyojaribu kusema. Yeye alisema, "Maono na vitu," kasema, "hayo ni ya ibilisi," akasema, "ama, yeye ni namna fulani ya kiini macho, ama anafanya kazi nje ya utambuzi wa hisi." Ulimwengu wa kielimu daima unajaribu kuliwazia Hilo.

61 Hapo ndipo walipojaribu kumwazia Yesu. "Unafanyaje mambo haya? Ni kitu gani kilichoyafanya haya?"

Akasema, "Nitakuuliza swali. Ilikuwa ni huduma ya Yohana Mbatizaji … Ilikuwa ni ya Mungu au ya mwanadamu?" Mnaona?

Kasema, "Hatuwezi kusema."

Kasema, "Wala mimi siwaambii." Hiyo ni kweli. Wakaendelea. "Tokea hapo hakuna mtu aliyemwuliza neno lolote." Mnaona? Yeye aliwakatilia mbali tu, hakuwaambia kitu kuhusu jambo hilo; si kazi yao. Alikuwa na kazi ya kufanya na akaimaliza.

Mungu na atusaidie kufanya jambo lile lile. Haitubidi kujibu maswali ya ibilisi, hiyo ni kweli, "Kama uko hivyo, fanya hivi na vile." Unawajibika kwa hiyo Injili, mhubiri anawajibika, na hivyo tu; si namna lilivyoandikwa, anawajibika tu kuisema.

Na kama mtumishi, kama wewe ni nabii, unawajibika kwa Mungu. Na kama maono yanayokuja yanaangazia Maandiko haya na kuonyesha ni kitu gani, wewe unawajibika kwa kila Neno lililo katika Biblia hiyo, maana yote yaliandikwa na watu kama wewe. "Mungu wa kale alitenda kazi, kwa manabii, na kuandika Taka …" Biblia Takatifu. Mnaona? Wala hakuna nabii halisi wa Mungu angeweza kukana Neno moja Lake, bali kuamini kila Neno na kuhubiri vile vile. Halafu basi Mungu anawajibika kutoka kwenye njia hiyo kulifanya Neno hilo litimie vile vile hasa lilivyoahidiwa, Mbegu itakua.

62 Sasa, angalia tena, upesi, tunaona hapa ya kwamba siku zote saba ambazo mkate huu ulipaswa kuliwa, kupitia Nyakati Saba za Kanisa. Sasa, wakati ilipaswa kufa na kuingia ardhini.

Na huyu mkosoaji aliyenizungumza kunihusu mimi, alisema, "Kuhusu Mungu ambaye ninyi watu mnamwabudu, ambaye angeketi kwenye zile Nyakati za Giza na kuwaangalia hao akina mama, waja wazito, baadhi yao wakiwa na watoto wachanga mikononi mwao, watu waaminifu, watupwe kwenye uwanja wa michezo nao simba wawararue vipande-vipande, huku wakipiga mayowe; wakawaangika misalabani na kuwachoma moto; wakawavua wanawake nguo, bikira wachanga, na kujirusha nyuma namna *hii*, na kuwafungulia simba wawashambulie." Kasema, "Mungu ambaye angeketi huko Mbinguni, anayedhaniwa kuwa kwenye kiti Chake cha enzi, na kuangalia chini na kusema Yeye anafurahia jambo hilo," kasema.

Halafu, mnaona, hiyo ni dhana ya kiakili ambayo ni ya ibilisi. Kama mtu huyo alikuwa wa kiroho, angalijua ya kwamba punje hiyo ya ngano haina budi kufa, ilibidi izikwe katika kanisa kuu la Kirumi.

63 Lakini basi chipukizi dogo la kwanza la Uzima lilitokea katika yale matengenezo ya Martin Luther, ya

kwamba, "Mwenye haki hataishi kwa mkate mtakatifu ambayo kasisi anatoa, bali kwa Neno la Mungu. 'Mwenye haki ataishi kwa imani!'" Lilichipuza vijitawi viwili. Ile punje ya ngano ikaanza kukua.

Ndipo akaja John Wesley na akaongeza kwenye hilo. (Kulikuwa na wengi wa hao wengine, ambao … Zwingli na hao wengine wakaja na kukana kuzaliwa na bikira, na ikafa tu.) Lakini moja kwa moja ikaja Methodisti, kishada, chavua, siku ya umishenari. Nao walihubiri utakaso; wakaongeza kishada.

Ndipo basi wakaja Wapentekoste katika kapi, zaidi sana, kuwadanganya Wateule. Inaonekana kama punje halisi ya ngano, ukiifungua, hakuna ngano hata kidogo. Lakini ule Uhai unapitia kwenye kapi.

64 Sasa, hivi mmeona, kila miaka mitatu baada ya mkutano m—mkuu, kile kinachotukia? Dhehebu. Hii ni miaka ishirini na hakuna dhehebu. Mwana-Kondoo mpendwa anayekufa, jalia kamwe lisifanye hivyo. Kama nikiondoka katika kizazi hiki, jalia watu wanaouamini Ujumbe huu kamwe wasilivumilie dhehebu! Mungu ataninii … Utakufa moja kwa moja kwenye njia yako! Kumbukeni hilo! Saa ile ile mtakayolitaja dhehebu miongoni mwenu, sijali ninyi ni waaminifu namna gani, kumchukua mwanadamu kama kiongozi wenu badala ya Roho Mtakatifu kulithibitisha Neno hili, hiyo ndiyo saa mtakayokufa! Mbegu halisi haiwezi, kwa maana hamna kitu kilichosalia baada ya mbegu, ni kitu kile kile kilichokuwepo hapo mwanzo. Ni Bibi-arusi aliyeanguka ardhini apate kuzaa punje ya ngano tena.

65 Angalia:

*… Siku saba utakula mikate isiyotiwa chachu …*

Na itakuwa pamoja na Bibi-arusi…

Sasa, ninyi watu mliokuwa na maskini huyo mama wa Kimethodisti aliyekuwa akipaza sauti, na kadhalika, ambapo mlishangaa "Kama hakunena kwa lugha, hatakuwa huko." Huo ni uongo! Alikuwa ni Roho Mtakatifu yeye yule uliye naye leo, bali alikuwa katika umbo la kishada, si kurudishwa kwa vipawa. Lakini siku zote saba, kula tu mkate usiotiwa chachu, Neno. Hao, huko nyuma, wale waliounda madhehebu, wamekufa. Wao ni ubua, watakusanywa tu na kuchomwa moto. Lakini Uhai unapita ukiendelea moja kwa moja. Na ni jambo gani linalotukia? Uhai wote uliokuwa kwenye ubua, kwenye kishada, kwenye kapi, wote unaishia kwenye ngano. Na Roho Mtakatifu yule yule aliyemleta Luther, akamleta Wesley, akawaleta Wapentekoste, akaishia katika Bibi-arusi kwenye ule ufufuo.

66 "Siku saba, mle mkate usiotiwa chachu." Hakuna chachu itakayoonekana miongoni mwa Bibi-arusi, ha—hakuna neno litakaloongezwa, hamna kitu. Kumbukeni, neno moja lilisababisha kila mauti yaliyoko duniani; kila mtoto haramu alizaliwa kwa sababu Hawa, lile kanisa la kwanza, bibi-arusi wa Adamu wa kwanza, alilishuku Neno la Mungu na kukubali mawazo Yake ya kidhehebu, ama ya kielimu, ama ya shule; kwa kuwa yalitolewa hoja, kwamba, "Hakika, Mungu ni Mungu mwema." Mungu ni Mungu mwema, bali Yeye pia ni Mungu mwenye haki. Hatuna budi kulitimiza Neno Lake! Shule, aliikubali.

Hapo ndipo baadhi yenu wavulana wa seminari, hapana shaka mkiwa na wito maishani mwenu, bali mnakimbilia shule fulani ya Biblia mpate kudungwa na fundisho hili, na hapo ndipo mnapokufia… Kaa na Mungu na Neno Lake. Hawatakuruhusu; ama, hata huwezi kuwa mshiriki wa kusanyiko lao, hawatakukubali jukwaani. Kwa hiyo acha waichukue, acha wafu wakawazike wafu, na tumfuate Kristo aliye Neno.

67 Sasa, siku saba hakutakuwa na chachu iliyochanganywa katika Bibi-arusi, Kanisa, siku saba.

Sasa angalia. Sasa kwa kuwa hakuna …

*Wala isionekane kwako chachu muda wa siku saba katika mipaka yako yote; ...* (Dhabihu hapa ni mfano: Bibi-arusi akitoka kwenye dhabihu ambayo ni Kristo.) *... wala katika hiyo nyama uchinjayo siku ya kwanza jioni, ...*

Na mnakumbuka—mnakumbuka jinsi ambavyo ndiyo kwanza tuzipitie Nyakati za Kanisa? Mjumbe wa kanisa daima huja tu mwishoni mwa wakati huo mwingine wa kanisa, daima. Kufa kwa Pentekoste kunaleta kunyakuliwa kwa Bibi-arusi. Mnaona? Kufa kwa Luther kulimzaa Wesley. Mnaona? Kufa kwa Wesley kulizaa Pentekoste. Kufa kwa Pentekoste kunaleta Ujumbe sasa. Hapa, liko papa hapa, limeainishwa kote katika Maandiko. Hakuna andiko katika Biblia lisilopatana moja kwa moja na lingine. Mnaona? Mifano hii yote. Sina elimu, bali nina Roho Mtakatifu anayenionyesha kupitia katika mkondo mwingine anayefundisha kutoka, kwa maumbile; na hiyo ni kwa Neno. Hapana budi kuwa ni Neno, mambo yaliyoahidiwa.

*… Nyama, … sadaka siku ya kwanza … jioni, kisilale chochote usiku kucha hata asubuhi.*

68 Sasa, hata Luther, ambaye alikuwa na ile Kweli na akalifundisha kanisa "wenye haki wataishi kwa imani." Hutaki kushikilia hilo kuwa ndilo fundisho kamili, katika wakati wa Kimethodisti. Utafanya nini? Iteketeze kwa moto. Mfano wa nini? Dhehebu linalotoka kwenye Neno hilo ni kapi, ubua, maganda, hayana budi kuchomwa moto. Hiyo sehemu ya kimadhehebu ambako imepitia haipaswi kusalia, haina budi

kufa. Usiiache mpaka kwenye mapambazuko ya mwingine—wakati mwingine, iteketeze! Yeye anazungumza sasa na Bibi-arusi hapa, Bibi-arusi tu, akija katika kila wakati.

Angalia namna ilivyo nzuri, "Damu ya mwana-kondoo." Hawa ndio Mwili wa Kristo, Dhabihu: damu ya mwana-kondoo mlangoni. Sasa, kumbukeni, mwana-kondoo alichinjwa ambaye alikuwa mfano wa Kristo.

Ama tungeweza kuchukua wakati mwingi, bali sina … dakika chache tu nyingine za kukaa hapa. Huenda ikanilazimu tu kusimama na kuanza tena usiku wa leo, mnaona, kwa kuwa tunachukua muda mrefu mno. Ni … Nina kurasa ishirini za hili hapa, za muhtasari, juu ya somo hili moja.

69 Angalia sasa, juu ya jambo hili, yule—yule mwana-kondoo alikuwa ni Kristo katika umbo la fumbo. Ama je! nililisema hilo vizuri? Mfano; Kristo alikuwa Mwana-Kondoo. Alikuwa awe ni wa kiume, wa kwanza kutoka kwa maskini mama kondoo; au kondoo jike, vyovyote utakavyochagua kumwita. Hana budi kuwa ndiye wake wa kwanza. Naye hana budi kujaribiwa kwanza kuona kama kuna hila juu yake.

Sasa, Kristo alijaribiwa; Mwana-kondoo kwanza kutoka kwa mama kondoo, Mariamu bikira. Na alijaribiwa na nini? Shetani dhidi ya Neno. Wakati alipomgonga Hawa, yeye alianguka; alipomgonga Musa, alianguka; bali wakati alipomrukia Kristo, na kujaribu kumnukulia Maandiko vibaya, a-ha, alikuta kwamba huyo hakuwa ni Musa. Mnaona? Yeye alijaribiwa. Ni nini kilichofanya … akageuka, akasema, "Kama Wewe ni Mwana wa Mungu. Sasa wananiambia Wewe unafanya miujiza, nao wananiambia ya kwamba Masihi atafanya hivyo. Sasa, kama ni, Wewe una njaa, hujala, geuza mikate hii kuwa, ama, mawe haya kuwa mikate, na ule."

Yeye alisema, "Imeandikwa, 'Mtu hataishi kwa mkate tu.'" Kanuni zako za imani, kadhalika. Lakini kwa nini? Kila Neno! Sehemu ya Neno? "Kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Hilo ndilo mwanadamu huishi kwalo. Mnaona? Mwana-Kondoo alijaribiwa, aone kama kuna mahali popote alipoanguka.

70 Mafarisayo, "Ee Rabi, Wewe Nabii kijana, tunafikiri Wewe ni mzuri sana. Wewe u mwema."

"Kwa nini kuniita mwema? Kuna Mmoja tu aliye mwema, na huyo ni Mungu. Je! Unaamini jambo hilo?"

"Loo, naam. Mungu."

"Vema, Mimi Ndiye, basi." A-ha. "Ulisema kuna Mmoja tu aliye mwema. Kwa nini mnaniita Mimi 'mwema,' wakati hamwamini mimi ni Mungu?" A-ha. "Kwa hiyo mbona unaniita mwema? Ni kitu gani kinachokufanya ufanye hivyo? Ni kitu gani kilichokuvuvia kusema hivyo, wakati unajua kuna mwema mmoja tu, na huyo ni Mungu?"

"Tunajua Wewe huna upendeleo kwa hadhi ya mtu wala neno la cheo chao. Tunajua hilo." Jaribu … Yeye alimjua huyo mnafiki. Mnaona?

71 Yeye alijaribiwa kuona mahali alipokuwa amesimama, mnaona, alijaribiwa katika kila namna, alijaribiwa kama vile sisi tunavyojaribiwa. Lakini Kwake Yeye, hakukubali kushindwa, hata kidogo. La, bwana! Huyo alikuwa ni Mwana wa Mungu.

Naye mwana-kondoo akajaribiwa, na akawekwa kwa siku kumi na nne. Hiyo ilikuwa ni Sabato mbili, ama nyakati mbili. Moja ni kwa ajili ya Wayahudi, ambapo walimtoa mwana-kondoo kama mfano; moja ni kwa Mataifa, ambao wana Mwana-kondoo halisi, na wote walikamilishwa kwa kuamini Mwana-kondoo huyu angekuja. Lakini alijaribiwa ninii kumi na nne…ama alichunguzwa siku kumi na nne, Yeye alikuwa ni Neno.

Nawe unaweza kuchunguza Agano la Kale, useme "Linalaani lile Jipya." Umekosea! Agano la Kale linashuhudia tu lile Jipya.

Mtu fulani alikuwa anataka kunipa changamoto si muda mrefu uliopita, kasema, "Ana shida gani?" Kasema, "Vema, hata anafundisha kutoka katika Agano la Kale." Mhubiri Mkristo, wazia jambo hilo. Kasema, "Agano la Kale limekufa na limekwisha." Loo, la! Loo, la! Ni mwalimu tu, linaonyesha yaliyoandikwa ukutani. Mnaona? Hiyo ni kweli.

72 Sasa, mnaona, siku kumi na nne alijaribiwa, huyo alikuwa ni Kristo. Sasa angalia, ndipo akauawa wakati wa jioni, alipaswa kuuawa, yule mwana-kondoo aliuawa. Kristo alikufa wakati wa jioni, alasiri. Na halafu angalia, ndipo yeye pia alikuwa …

Ile damu ilipaswa kuwekwa kwenye miimo ya milango, mnaona, ambayo damu ni uhai wa mnyama. "Mtakula nyama yake; bali damu yake ambayo ni uhai, imwageni." Mnaona? Ilikuwa iwe … Damu ilikuwa ipakwe kwenye vizingiti vya miimo ya mlango wa nyumba ambamo sadaka hiyo ilikubalika. Utukufu! Uhai ni nini? Jina. Hiyo … Aliweka jina la mtu huyo … Nenda mlangoni, na uangalie, uone ni jina gani mlangoni kabla hujapiga kengele. Mnaona? Ile damu iliwekwa kwenye kizingiti cha mlango kama mfano wa ile sadaka iliyokuwa ndani.

Sasa tutapata mahali pa kuabudia, moja kwa moja kupitia pale, tukipitia kwenye hiyo Damu. Angalieni, ile damu kwenye mlango ilikuwa ikizungumzia lile jina la kile kingeninii…kilichokuwa ndani, walikuwa mle ndani. Mahali petu pa kuabudia, Mwana-Kondoo, ni Neno. Tunajua jambo hilo.

73 Sasa, kifungu cha 4, angalieni, "Msiache mkate wowote, msiache chochote cha dhabihu hiyo," ama, kuchukua moja kutoka kwenye wakati mmoja hadi mwingine.

Jaribu kurudi nyuma na kusema, "Vema, sasa, sisi ni Walutheri, tunataka kuja hapa juu," hamna budi kufa kwa wakati wa Kiluteri kuzaliwa katika wakati wa Wesley. Huna budi kufa katika wakati wa Wesley upate kuzaliwa katika wakati wa Kipentekoste. Nawe huna budi kufa kwa wakati wa Pentekoste, usiache chochote chake kilichosalia, uviteketeze kwa moto, kwa maana itachomwa kama ubua ambamo ngano inatoka. Ubua, dhehebu, halina budi kuchomwa moto. Kwa hiyo usilete dhehebu lako katika Ujumbe mpya. Hili ni Neno sasa. Huo ndio uliounda dhehebu, ubua; ulilibeba, hiyo ni kweli; bali likaja likaingia huku, ndipo huo ubua ukafa. Lilikuwa ni bebaji, dhehebu hilo, bali Neno linaendelea moja kwa moja mbele. Naam, Neno linaendelea moja kwa moja.

74 Sasa chukua kifungu cha 5 na cha 6. Angalia, "Si …" Sasa hebu tuchukue kifungu cha 5 na cha 6.

*Usimchinje pasaka ndani ya malango yako yote akupayo BWANA, Mungu wako;*

Sasa kumbukeni, "Si kwenye lolote la malango haya." Bwana anawaruhusu kuwa na madhehebu haya, mnaona, "malango haya."

Ila mahali atakapochagua BWANA ... Mungu wako, apakalishe jina lake, ...

Hilo ndilo Lango, mahali pekee. "Si katika lolote la malango haya." Lakini Mungu ana Lango.

75 Unasema, "Kila asubuhi ninaingia kwenye lango la Kimethodisti." Hilo ndilo kanisa. "Kila asubuhi ninaingia kwenye lango la Katoliki." A-ha. Vema, Bwana anawaaruhusu watu Wake waingie na kutoka kwenye malango hayo. Mungu ana watu katika kanisa Katoliki, kanisa la Kimethodisti, kanisa la Kipresbiteri, wote hao, Wapentekoste. Hakika, lakini usininii … humwabudu Bwana katika lango hilo. Mnaona? Lakini Bwana ana lango fulani. Utukufu! Yeye ana lango.

*Ila mahali atakapochagua Bwana, Mungu wako,…apakalishe jina lake, ndipo… mtakapomchinja pasaka jioni,…*

76 Rebeka alimpata Isaka wakati gani? Ni wakati gani Eliezeri alimwita awe bibi-arusi? Wakati wa jioni!

Itakuwa Nuru yapata wakati wa jioni,
Njia ya Utukufuni hakika mtaipata;
Katika njia hiyo ya maji kuna Nuru leo,
Kuzikwa katika Jina la thamani la Yesu;
Vijana kwa wazee, tubuni dhambi zenu zote,
Roho Mtakatifu hakika ataingia;
Nuru za jioni zimekuja,
Ni ukweli kwamba Mungu na Kristo ni mmoja.

Huo ulikuwa ni mwanzo Wake, sasa ametoweka akaingia kwenye Nuru ya Bibi-arusi. Mnaona ninalomaanisha?

77 Afadhali nifunge hapa, nianze tena usiku wa leo, maana sitaki mliache hili, mnaona. La, la, ni—ni wakati wa chakula cha jioni. Vema, vema, nina mambo mengi mno niliyoandika hapa. Loo, jamani! Vipi kuhusu usiku wa leo, hilo lingekuwa ni bora zaidi? [Kusanyiko linasema, "La. Sasa." — Mh.] A-ha? Vema, kama wewe … Unataka kujaribu zaidi kidogo? ["Naam. Amina."] Vema, hebu twende mbele kidogo basi, tutaharakisha upesi sana. Na hilo je?

78 Sasa, ingia katika nini? "Hutaingia kwenye lango lolote ambalo Bwana Mungu amekupa, bali kwenye lango ambalo Bwana ataliweka Jina Lake." Si kuingia katika nyumba ya—ya lango ambalo ni mlango. Hiyo ni kweli? Mungu atalikalisha Jina Lake mlangoni, nawe hutaninii… Hilo ndilo lango linaloingiliwa kwenda mahali pa kuabudia, madhabahuni. Huingii mle ndani ukiwa na dhabihu yako kwenye lo lote la malango haya, bali katika lile lango ambalo Bwana Mungu huchagua kuliweka Jina Lake mle. Mnaona?

Sasa, Yeye amefanya hivyo? Lango hilo liko wapi? Katika Yohana Mtakatifu 10, Yesu alisema, "Mimi ndimi Lango, Mlango. Mimi Ndimi Mlango wa Nyumba ya Mungu. Mimi ni Mlango wa zizi la kondoo." Si zizi la mbuzi, zizi la kondoo. Mnaona? "Mimi Ndimi Mlango wa zizi la kondoo. Mtu anaweza kuingia katika Mlango huu, awe salama."

79 Na sasa tungeweza kukaa muda mrefu juu ya jambo hilo. Lakini, kuokoa wakati, Yeye Ndiye Mlango wa zizi hilo la kondoo. Sasa, tunataka kuona hapa. Vivuli na mifano kweli inaonekana wazi hapa, bali mimi…kama nikiuchukua ukurasa huo ningeninii…itawaweka kwa muda.

Vema, angalieni, hili linamwonyesha wazi kabisa, Yesu Kristo. Kwa maana Agano la Kale lote ni mfano Wake, sikukuu zote, ibada zote, na kila kitu. Nami nimeandika hapa chini, chini ya mistari hii ya Maandiko, "Eleza jambo hilo." Hapo ndipo itachukua muda mrefu. Eleza jinsi karamu zote … Hata sadaka ya unga ilikuwa ni mfano wa Kristo. Hebu na tuichukue hiyo tu.

80 Wakati mmoja kulikuwako na—na shule iliyoitwa shule ya wahudumu, ama shule ya manabii. Waliwafunza, wakawaelimisha manabii. Basi palitokea nabii halisi aliyeitwa na Mungu, aliyeenda kuwatembelea wakati mmoja. Vema, walitaka kumpa nabii huyo mzee heshima kidogo, kwa hiyo mmoja wao akatoka akaenda akachuma lundo kubwa la kile alichodhani ni njegere; bali zilikuwa ni matango sumu, naye alikuwa akitaka kuwalisha wote kwa hayo.

Loo! Tumekuwa na mapaja mangapi ya seminari! Mnaona? Sawa. Wanapika kitu fulani. Mnaona? Wana mapaja yaliyojaa ya Methodisti, mapaja yaliyojaa ya Baptisti, mapaja yaliyojaa ya Pentekoste. Lakini, mnaona, ni maotea ya pili, vile vinavyoweza kupogolewa kutoka mtini. Mnaona, si katika Mzabibu wenyewe. Tukizaa malimao, balungi, na kadhalika; si machungwa, bali yakidai kuwa machungwa.

81 Angalia tena. Sasa, katika hili—katika hili, wakati Eliya alipokuja na kuyaangalia, na kuona ya kwamba yalikuwa ni matango sumu ambayo yangemwua kila mmoja wao, walisema, "Ole wetu, tuna mauti katika chungu!"

Akasema, "Nileteeni konzi ya unga." Naye akatia unga ndani yake, akasema, "Sasa ni sawa, kuleni mtakayo." Ilibadilisha mauti yakawa uzima.

Na sadaka ya unga aliyotowa kwa Kristo … Yeye alikuwa ndiye sadaka ya Unga, na hiyo sadaka ya unga haina budi kusagwa kwa kinoo cha aina fulani kilichosababisha kila bonge la unga kuwa sawa, ikionyesha ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Yeye ni kitu kile kile cha kuweka katika madhehebu yako na yataishi: lile Neno! Kristo ni Neno, mifano yote ya kila kitu: maskani, m—m—mkate wa wonyesho, kila kitu. Ule mkate wa kosha uliovunjwa chini ya sahani ulikuwa ni mwili Wake uliovunjwa, ambao Wayahudi wangali hawawezi kuelezea ni kwa nini wanafanya hivyo. Mnaona? Na mambo haya mengine yote yalikuwa mfano Wake.

82 Sasa, basi, Yeye akionyeshwa wazi, tunaona sasa madhehebu yote na kanuni za imani zimeachwa nyuma; kwa kuwa Yeye Ndiye Neno safi la Mungu, lisilobadilika, ambalo ndilo mkate usiotiwa chachu, Yohana Mtakatifu 1. Hiyo ni kweli, Yeye ndiye Mkate usiotiwa chachu. Kwa hiyo wakati unapoongezea hiki ama kuongeza kile, ni chachu iliyoongezwa kwa Kile ulichopewa hapo awali.

Angalia hapa. Ni kitu gani kinachoua siku hizi? Wao huchukua na kuvizalisha chotara. Na unapovizalisha chotara unaviua. "Loo, linaonekana ni zuri zaidi." Hakika! Mahindi chotara; bisi, nafaka zingine zote zinazotokana na mahindi. Mahindi chotara: ubua mkubwa mno, mrefu, wa kupendeza, na mashuke makubwa mno, yanaonekana mazuri maradufu kuliko hayo mengine. Lakini ni mauti! Sayansi hata iligundua hilo. Mnaona? Usiyazalishe chotara, yatakuua.

83 Sasa, hapa, hebu niwaonyeshe. Juzijuzi nilikuwa ninamwagilia maua uani mwangu. Naye bibi huyo alikuwa na maua chotara yaliyokuwa kwenye chungu kidogo hapa, ama kipandio kidogo kando ya nyumba. Inatupasa kuvimwagilia vitu hivyo maji angalau mara tatu kwa juma, ama nne, la sivyo vitakufa. Na hapo palisimama mmea wa asili uani. Haijanyesha kule kwa muda wa miezi sita, kukavu tu… Kama kukinyesha, katika dakika kumi unaweza kuyapulizia mavumbi. Lakini maskini jamaa huyo amekaa pale, anapendeza zaidi na kunawiri zaidi kuliko chotara alivyokuwa na maji hayo yote. Ukimwondolea hayo maji, atakufa. Lakini alipata wapi maji yake? Na jambo lingine, inakubidi kuendelea kuyanyunyizia kila baada ya siku moja ama mbili, kuyakinga na chawa. La sivyo, chawa watammaliza, ni mwororo sana na laini. Bali hakuna chawa atakayelishambulia lile la asili. La, la! Atatambaa kwake kisha atambae aondoke. Yeye ni wa asili! Mnaona kile kuchanganya mbegu kumefanya?

84 Hilo ni jambo lile lile kanisani. Wanajaribu kuchanganya dhehebu na Neno, kufanya ninii … kujaribu kulifanya Neno liseme yale dhehebu linasema. Na unapofanya hivyo, inakubidi kuwanyunyizia, na kuwabembeleza, na—na kuwapa nyota za dhahabu kuja kwenye shule ya Jumapili, na cho chote kile. Hiyo ni kweli. Wakati, Mkristo halisi, aliyezaliwa mara ya pili, aliyezaliwa na Neno la Mungu, yeye ni mgumui. Huyo ni wewe. Chawa na mambo ya ulimwengu hayamsumbui. Yeye ni tai, huruka moja kwa moja kupita hayo. Mnaona, anapaa mbinguni. Mnaona? Ni kweli. Hakuna kitu …

85 Angalia. Sasa, hatuna budi kuelewa kwamba hapa, dhehebu, kanuni za imani, na chochote kinachoongezwa cha mkate uliotiwa chachu hakiwezi kuchanganyikana na mkate usiotiwa chachu. Nayo Biblia inaliainisha hapa katika sakramenti, ya kwenda kuabudu, kwamba hakuna chachu unayoweza kwenda nayo, na Mungu aipokee.

Unasema, "Mimi ni Mmethodisti." Papo hapo unakufa! "Mimi ni Mpentekoste." Unakufa!

Mimi ni wa Kristo. Hiyo ni kweli. Huna budi kusimama juu ya kitu fulani. Hiyo ni kweli. Una—unasimama juu ya kitu fulani.

Churchill wakati mmoja alisema, aliinua vidole viwili na kusema, "Tumepata ushindi." Na Uingereza ikashikilia jambo hilo, wakamwamini Churchill.

Na uamini usiamini, asubuhi ya leo, unasimama kwa kitu fulani. Kuna kitu kimoja tu unachoweza kuishi na kusimama nacho, na hicho ni Kristo, lile Neno. Kweli!

86 Angalia, hakuna kitu katika Biblia kinachofananishwa na madhehebu ila Babeli. Na Babeli ilianzishwa na Nimrodi, na Nimrodi alikuwa ni haini. Naye alikuwa na kundi la wanawake mle ndani, waliopaswa kuwa ni malkia wake, huyo alikuwa nabii mke. Hata wanafikiri ya kwamba Balaamu wa kale alitoka sehemu hiyo, walikuwa na mizizi na kadhalika. Waliabudu, mwajua (wengi wenu wasomi mnaosoma Babeli Mbili kilichoandikwa na Hislop, na kadhalika, na historia ya kanisa), na namna wa—walivyofanya. Nao walikuwa na wanawake waliofanya jambo hili, na wanawake … mungu mke, na kila kitu, na ilikuwa ni dini ya kulazimisha. Kila mtu, kila mji uliozunguka Babeli ulilazimishwa kuja Babeli kuabudu chini ya Nimrodi kwenye ule mnara. Mnaona? Hiyo ni kweli. Walilazimishwa kufanya hivyo, kwa Babeli. Hapo ndipo mchafuko ulipotokea.

Na hivyo hasa ndivyo kanisa lilivyo leo, "Usipohudhuria shule ya Jumapili, usipofanya hivi, na inatupasa tukulipe ufanye hivi na ufanye hivi na ufanye vile, huko tena."

87 Kule nje huko Tucson, wanasikiliza asubuhi ya leo, wakati mmoja nilishangaa … Daima nimewahimiza watu, "Nendeni kanisani, haidhuru mnaenda wapi." Nami nimewaona watu kwa namna fulani wakirudi nyuma, na wakienda *namna hii.* Ndipo nikawaza, "Kuna nini?"

Nikawaendea baadhi yao, "Siku ya kwanza ukiwa hapo, watakujia, 'Jiunge na kanisa letu.' Usipofanya hivyo, hukaribishwi." Mnaona? Mnaona? Ni jambo la kulazimishwa, limelazimishwa, mnaona, na hilo ni Babeli. Lakini katika Kristo, unaingia kwa kuteuliwa; si kwa nguvu, moyo wako unakuingiza ndani.

Mungu hakuweka Jina Lake wakati huo katika Babeli. Kwa makini sasa. Yeye hawezi kuweka Jina Lake katika Babeli, makanisa. Loo, wao, wanaweka Jina Lake mle ndani, bali Yeye kamwe hakuliweka. La.

88 Unasema, "Vema, sasa, Ndugu Branham!" Ngojeni, ngojeni, kaeni kimya tu kwa dakika moja. Mliniomba nikae kidogo. Hivi hamwezi kuona? Sasa angalia, waliweka Jina Lake mle, bali Yeye hakuweka.

Sasa, Yeye alisema, "Mahali nitakapokutana nawe na kupokea dhabihu yako ndipo ni pale nilipopachagua kuweka Jina Langu. Unaingia kwa lango hili, mlango huu ambapo nilichagua kulikalisha Jina Langu. Hapo ndipo unapokuja."

Vema, waliweka, "Hili ni kanisa la Kristo." Kama kuna kitu walichokosea katika azimio hilo, ni kuacha neno: "mpinga." A-ha, yote aliyofundisha, wanayakataa. Mafarisayo wa kisasa.

89 Lakini hatuna budi kutafuta mahali ambapo Yeye aliweka Jina Lake, kwa kuwa ndani Yake mna lango Lake pekee lililowekwa. Amina! Utukufu! Angalia! Yeye aliweka wapi Jina Lake? Katika Mwanawe.

"Loo," unasema, "sasa ngoja kidogo, Ndugu Branham. Huyo alikuwa ni Mwana, si Baba."

Mwana daima huchukua jina la baba yake katika kila hali. Nilikuja hapa duniani kwa jina la Branham kwa sababu jina la baba yangu lilikuwa ni Branham.

Yesu alisema, "Nilikuja katika Jina la Baba Yangu, wala hamkunipokea." Mnataka Maandiko juu ya jambo hilo? Yohana Mtakatifu 5:43. Mnaona? "Ni—nilikuja katika Jina la Baba Yangu, wala hamkunipokea." Ndipo Baba akaweka Jina Lake Mwenyewe, ambalo ni "Yesu," katika Mwana. Naye Ndiye Njia, Yeye Ndiye Mlango, Yeye ni Nyumba, Yeye ni mahali ambapo Mungu alichagua kulikalisha Jina Lake. Mungu kamwe hakuweka Jina Lake ndani yangu, kamwe hakuliweka kanisani, kamwe hakuliweka katika Methodisti, Baptisti, Katoliki, bali aliliweka katika Kristo aliye Imanueli Mpakwa Mafuta.

90 Nalo Jina limo katika Neno kwa sababu Yeye ni Neno. Amina! Yeye ni nini basi? Neno lililofasiriwa ni dhihirisho la Jina la Mungu. Si ajabu. "Mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia hili, kwamba Mimi ni Nani. Na juu ya mwamba huu nitajenga mahali Pangu pa kuabudia, wala malango ya kuzimu hayawezi kupatikisa." Amina! Enyi Kanisa la Mungu lililo hai, simameni katika msingi thabiti juu ya Yesu Kristo pekee. Unaweza kuimba wimbo huo, lakini kama wewe hauko juu ya Kristo Neno, wewe ni mchanga unaopepesuka, unaoyumbayumba. "Lakini juu ya Mwamba huu," Kristo, "Neno Langu."

91 Yeye aliujenga ujumbe wa Kilutheri nao wakauundia dhehebu. Ulikuwa ukikua, mahali pa kuwekea miguu. Ndipo akakua mpaka sehemu ya mguu, Methodisti, na kadhalika. Hapo ndipo Yeye alipolijenga Kanisa Lake, juu ya Neno Lake! Sasa, Yeye si mguu wote wala paja lote, Yeye ni mwili; na sasa ni sehemu ya kifuniko. Mliona katika piramidi? Ambapo, mimi sihubiri dini ya piramidi, sasa.

Lakini Biblia ya kwanza kuwahi kuandikwa, iliandikwa angani, zo- … [Sehemu tupu kwenye kanda —Mh.] Mliona jambo hilo? Linaanza na bikira, umbo la kwanza katika zodiaka. Umbo la mwisho ni Leo yule

simba. Yeye alikuja kwanza kwa bikira, Anakuja kama Simba wa kabila la Yuda. Kabla tu ya hapo, wakati wa kaa, samaki waliokingama, nyakati hizo zingine zote. Kama tungalikuwa na wakati wa kuzipitia zote; ambao tunao, huko maskanini.

92 Nayo pira-…piramidi ikiwa ni ile misingi, kufikia juu kwenye kile chumba cha mfalme. Na kabla tu hujafikia kwenye ukuta wa saba, kuna ubao mdogo mnene wa utambulisho pale, ambapo mjumbe anatoka kuja kukuleta kwa mfalme. (Mjumbe, Yohana Mbatizaji, ambaye alimtambulisha, kwa Mfalme.) Lakini lile Jiwe la Kichwa lilikataliwa. Nao hawajui, Jiwe la Skonzi, ama chochote kile, hawajui mahali liliko, kwa sababu ni jiwe lililokataliwa. Lakini hilo ndilo jiwe linalofunika kitu hicho chote, linaloifanya piramidi kupitia nyakati zote saba za kanisa. Ongeza neema, ongeza *hii*, ongeza *hii*, kuna nyongeza saba, ya mwisho ni Kristo. Ongezea *hii* kwenye upendo wako, ongezea neema kwa neema yako, ongezea kitu kingine, na kitu kingine, mpaka inafikia kwa Kristo aliye Jiwe la Kichwa, "Nami Ndimi Mlango."

93 Sasa, mwana daima huja katika jina la baba yake. Mwana yeyote huja katika jina la baba yake. Naye Yesu alisema, "Nilikuja katika Jina la Baba Yangu." Basi Jina la Baba ni lipi? Jina la Mwana ni lipi? Naye akasema, "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona." Naam, Yeye amekuja katika umbo la Roho Mtakatifu, Hilo Jina ni Yesu. Hiyo ndiyo sababu walikuwa wakiabudu, "Ee Yesu!" Mnaona? Mnaona? Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu: Ni Bwana Yesu Kristo. Hivyo tu. "Nimekuja katika Jina la Baba Yangu, wala hamkunipokea."

94 Sasa, kumbukeni, Yeye pia aliongezea hapa na kutuonya, "mwingine atakuja," madhehebu, kanuni ya imani. "Watakuja katika jina lao nanyi mtawapokea. Hamtanipokea, Neno lililothibitishwa na kuhakikishwa mbele zenu."

Kama alivyokuwa wakati huo, ndivyo alivyo leo. Msikose jambo hilo, watu kote katika taifa hili! "Mwingine atakuja, kanisa, nanyi mtamwamini huyo, kwa sababu mnaweza kufanya vyovyote. Sitalithibitisha." Yeye kamwe (wakati wowote, kamwe) hakuthibitisha kitu chochote (katika kanisa lolote) nje ya Ujumbe uliotolewa: wa Luther, kuhesabiwa haki; Wesley, utakaso; Pentekoste, kurudishwa kwa vipawa. Baada ya … Na mara wanapoliundia dhehebu, hapo likafa. Yachunguzeni Maandiko.

95 Lakini Yeye alisema, "Nitachagua mahali pa kuweka Jina Langu." Na Jina hilo lilikuwa ni Yesu. Na Yesu ni Neno, Yohana Mtakatifu 1. Hiyo ni kweli? Hapo ndipo mahali pa kuabudia, katika Kristo Neno. "Nimekuja katika Jina la Baba Yangu."

Nabii alisema, "Jina Lake ataitwa Imanueli." Hiyo ni Mathayo 1:23, kama unataka kuandika hilo. Yesu, Yehova, Mwokozi.

Sasa, aya ya 5 inaonyesha ya kwamba Yeye ndiye Mlango. Kwa sasa, thibitisho nyingi zisizoonekana, Lango hili, na Jina, na mahali hapa panaweza kuthibitishwa ya kwamba kuna mahali pamoja tu ambapo Mungu hukutana na mwanadamu kuabudia, na hapo ni wakati akiwa ndani ya Kristo.

Sasa, sasa swali ni, "Tunaingiaje ndani Yake?" Sasa, huenda hili likaumiza kidogo tu; lakini, mwajua, kama vile kunywa dawa, kama haikuchefui, haikusaidii kamwe. Mnaona?

96 Sasa, Walutheri walitaka kuingia kwa njia moja, kwa kujiunga na kanisa la Kilutheri. Mmethodisti ilitaka kuingia kwa kupiga makelele. Wapentekoste walitaka kuingia kwa kunena kwa lugha. Hilo bado silo! Mnaona? La, hizo ni karama, na kadhalika. Lakini Wakorintho wa Kwanza 12 inasema, "Kwa Roho mmoja." Roho wa Mungu, ambaye ni mpaji Uzima kwa Neno (Mbegu), kuithibitisha hiyo Mbegu kwa ajili ya majira hayo. Mnaona?

Hii hapa mbegu ya wakati wa Kimethodisti imekaa hapa, ilihitaji Roho Mtakatifu kuifanya mbegu hiyo ichipuke na kusafi-…kulisafisha kanisa kwa utakaso; Luther hakuhubiri huo, maana hakuujua. Wapentekoste walitaka kunena kwa lugha kwa ajili ya kurudishwa kwa karama. Kila mmoja anatangaza, "Hilo ndilo! Hilo ndilo!" Mnaona?

97 "Lakini kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja," na Mwili huo ni familia, familia ya Mungu. Na hiyo ni Nyumba ya Mungu, na Nyumba ya Mungu ni Jina la Yesu Kristo. "Jina la Bwana ni ngome imara, wenye haki huikimbilia wakawa salama."

Sasa, utaingiaje kwa cheo? Hundi yako itapokelewaje kwa kusema, "I—ilipiwe Kasisi, Daktari, Mhudumu."? Mnaona? Mnaona? Huenda ukawa mchungaji, daktari, mhudumu. Lakini *jina* la Bwana ni "Yesu Kristo." Mnaona?

"Nimechagua kuweka Jina Langu kwenye mlango wa nyumba ya ibada Yangu, kwa kuwa familia Yangu itakusanyika mle ndani chini ya Damu; kama ilivyokuwa huko Misri, kitu chochote kilichokuwa nje kilikufa. Na ndani humo hamna mkate uliotiwa chachu! Hakuna mchanganyiko wa kimadhehebu ndani Yake mahali popote, nyumba Yangu! Watoto wangu, waliozaliwa kwa jeni Zangu!" Amina! Utukufu kwa Mungu! "Jeni zangu zimo ndani yao! Jamani … Niliweka Neno Langu ndani yao. Nitayaandika juu ya vibao vya mioyo yao. Hiyo ndiyo familia Yangu, familia ya Mwili wa Yesu Kristo; ile familia. Na mlango huu utaingia, si

Methodisti, Baptisti, au Pentekoste, bali katika mlango ambapo nitaweka Jina Langu." Siyo Methodisti. Jina la Mungu si Methodisti. Jina la Mungu si la Kipentekoste. Jina la Mungu si Baptisti. Jina la Mungu si Katoliki. Kaa nje ya milango basi. Mnaona? Mnaona? Mnaona?

98 "Lakini mahali ambapo nimechagua kuweka Jina Langu." Sasa, hakuna mahali pengine katika Biblia palipowekwa ambapo Mungu alipata kuliweka Jina Lake, ni katika Yesu Kristo tu, kwa kuwa Yeye ni Mwana wa Mungu akilichukua Jina la Mungu, na Jina la kibinadamu la Mungu. "Na hakuna jina lingine lililotolewa chini ya Mbingu ambalo huna budi kuokolewa kwalo." Sijali, Methodisti, Baptisti, Presbiteri, katekisimu, ama cho chote unachotaka kufanya; ni kwa Jina la Yesu Kristo tu ambapo kila goti litapigwa na kila ulimi utakiri, Yeye akiwa Bwana. Hivyo ndivyo unavyoingia.

Na kama ulibatizwa tu kwa maji—sawa, halafu unalikana Neno, basi wewe ni haramu; kuzaliwa kwako hakukuwa sahihi. Unadai ya kwamba ulimwamini Yeye basi, na unamkana.

Ningewezaje kuikana familia yangu? Wakati … Ningewezaje kumkana Charles Branham kuwa ni baba yangu? Uchunguzi wa damu mlangoni unaonyesha jambo hilo. A-ha.

99 Tendo langu, na thibitisho la Neno la Mungu maishani mwangu linaonyesha kama mimi ni mwana wa Mungu ama la. Sasa, hapo ndipo mahali pekee pa Mungu. Mnaona? Mahali pekee ambapo Mungu atapokea dhabihu yako (sijali wewe ni mwaminifu namna gani) ni katika Kristo.

Na kumbukeni … Unasema, "Vema, niliamini; Niliingia, pia." Kumbuka, Biblia inasema … Mnasema, "Vema, Biblia ilisema, 'Kila aaminiye ya kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, ameokoka, ataokoka.'"

Inasema hivyo, lakini kumbuka pia imeandikwa, pia imeandikwa, "Hakuna mtu awezaye kumwita Yesu Kristo, ila kwa Roho Mtakatifu." Mnaona? Huenda ukasema "Ndivyo alivyo," bali Siye mpaka Roho Mtakatifu Mwenyewe ambaye hulitia Neno Uzima alihakikishe hilo kwa kuthibitisha ya kwamba wewe ni mwana wa Mungu. Hayo ni Maandiko.

100 "Mahali ambapo nilichagua kuweka Jina Langu. Hutaabudu katika lango lingine lolote, bali penye lango nililokalisha Jina Langu; ndipo nitakupokea, wewe uko katika familia Yangu."

Sasa, familia ya Mungu inatii agizo la Baba wa familia. "Naye ni Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa milele; na milki yake na utawala havitakuwa na mwisho, uweza wa kifalme utakuwa begani Mwake." Naye akiwa Gavana, Mfalme, Imanueli, wa Kwanza, wa Mwisho, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa milele, kila mmoja wa watoto Wake hutii kila Neno kwa utaratibu kwa sababu wao ni sehemu Yake.

101 Tunaishi nyumbani mwetu kama wana Branham wanavyoishi. Unaishi nyumbani mwako, akina Jones, kama vile akina Jones wanavyoishi.

Na katika Nyumba ya Mungu tunaishi kwa Neno la Mungu na kila Moja litokalo kinywani mwa Mungu; na mwingine yeyote, mdanganyifu, hatutamsikiliza. Mnaona? "Mtakula mikate isiyotiwa chachu, kila wakati wa kanisa, kama tu ninavyowapa ninyi." Lakini msijaribu kurudi na kuingiza hilo kwenye Hili, kwa sababu imefikia kwenye ubua. "Mtachukua mifupa na vitu vilivyosalia kwenye sadaka na kuvichoma moto!" Umekwisha, wakati wa kanisa ulikufa, ukaendelea; tuko katika mwingine sasa. Amina!

"Mahali ninapochagua kuweka Jina Langu." Loo, jamani! Wakorintho wa Kwanza 12.

102 Angalia, Waefeso 4:30.

> *… Msimhuzunishe huyo Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa yeye mmetiwa muhuri hata … (ufufuo ujao?) … Hata siku ya ukombozi wenu.*
>
> *… Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu.*

Sasa angalia. Hebu na tulitumie hilo kwenye somo letu la Maandiko. Ndipo afadhali twende; Nafikiri ninawachosha watu. Mnaona? [Mtu fulani anasema, "La, sivyo, Ndugu Branham." — Mh.] Angalia hapa, watu wakiamka na kwenda nyumbani, mnaona, kwa hiyo wana—wana chakula cha jioni cha kupikwa, na mtu fulani wanayetaka kukutana naye. Hawakutarajia kuja hapa chini kusikiliza siku nzima. Mnaona? Lakini, angalia, unajua ninii …

103 [Ndugu Ben Bryant alisema jambo fulani — Mh.] Ben, loo, ninapaswa kukushughulikia! Ubarikiwe! Asante, Ndugu Ben. Ninakupenda, Ndugu Ben.

Laiti mngalijua yale mvulana huyo aliyoteseka kwa ajili yetu kwenye vile vita; amepigwa risasi kwelikweli, akalipuliwa, na chochote kile. Yeye amekuwa na maisha ya kila kitu, lakini Mungu amembariki. Yeye alidumu mwaminifu. Mkewe alimwacha, akakimbia na kuolewa tena, na kuwachukua watoto wake. Loo, jamani, siwezi kabisa kuliwazia.

Lakini, hata hivyo, Mungu akubariki, Ben.

Yeye amekaa sasa hivi amejaa marisau, yakizisukumiza neva zake na kila kitu kingine. Ambapo, inakubidi kujua asili ya mambo, mnaona. Mungu ambariki mvulana huyo. Ndiyo.

> *… Ambaye kwa yeye mmetiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu.*

104 Angalia! Sasa hili huenda likaumiza kidogo tu, bali angalieni. Msinikasirikie. Kumbukeni tu.

Wakati Israeli wakati mmoja walipouangalia mlango huo, huku damu hiyo ikiwa mlangoni, jina (ile damu, uhai), na kuingia chini ya damu hiyo, kamwe hawakutoka tena mpaka walipoondoka Misri.

> *…msimhuzunishe yule Roho mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa yeye* mnaingia wala hamtoki tena hata siku mtakayokombolewa.

(Mnaona?)

Mnajua, Biblia daima ni sahihi. Yeye huyaweka Maneno Mle, inakubidi kuyaweka mahali yanapoenda, kuifanya, kufanya picha yote ya ukombozi. Mnaona? Mnaona?

> *… Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa yeye mmetiwa muhuri hata siku ukombozi wenu.* (Mpaka umekombolewa.)

105 Umetiwa muhuri mle ndani, uko chini ya ile Damu. Hutoki tena. Na basi wewe ni nini? Mwana wa Mungu katika familia ya Mungu, ametiwa muhuri na Roho Mtakatifu. Ibilisi asingeweza kukupata hata afanyeje; kwa kuwa wewe umekufa, sehemu yako ya mume wa kale imekufa; nawe umezikwa, na uhai wako umefichwa katika Mungu kwa njia ya Kristo, na kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu. Mnaona? Yeye atakupataje? Utatokaje? Uko hapo! Utukufu! Sasa nitaacha hilo peke yake; vya kutosha tu mpate kujua ninalozungumzia.

106 Halafu kiumbe kipya, si kwa madhehebu bali kwa Neno. Wewe ni uumbaji wa Neno. Kwa kuwa jiwe la msingi liliwekwa ndani yako kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, mkachaguliwa tangu zamani kuwa wana na binti za Mungu.

Na juu ya hili likaja jiwe juu ya jiwe, katika kila wakati, kuthibitisha hilo Neno linalokuja, kama tu vile Yesu alivyofanya katika wakati Wake, ambao ni Jiwe la Kifuniko juu ya yote. Katika Yeye mlikaa kila kizazi. Katika Yesu kulikuwa na Musa. Katika Yesu kulikuwa na Daudi. Katika Yesu mlikuwako manabii. Hiyo ni kweli? Hebu mwangalie Yusufu, aliuzwa kwa karibu vipande thelathini vya fedha, akatupwa ndani, akadhaniwa amekufa, akatolewa nje, akaenda na akaja kwenye mkono wa kuume wa Farao. Angalia, hasa, Yesu alikuwa … Yusufu alikuwa ndani ya Yesu.

Na wakati alipokuja, Yeye alikuwa utimilifu wa wafalme, manabii (haleluya), Uungu kwa jinsi ya mwili ulikaa ndani Yake. Yeye alikuja kukomboa kutoka humo Bibi-arusi, Kipeo. Kipeo kinachomwambia Shetani kwamba …

Anaposema, "Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama mambo haya mnayozungumzia."

"Rudi nyuma yangu, Shetani." Mnaona? Mnaona, Kipeo kimesimama na kinalinda.

107 Wakati mwingine lile Jiwe la Kifuniko litarudi, kichwa cha hayo yote, na kumpokea Bibi-arusi Kwake; ambapo mwanamke anatolewa kutoka kwa mwanamume, sehemu ya mwanamume. Kila … Jeni za mwanamume zimo ndani ya mwanamke, ndizo zinazomfanya mwanamke. Na hivyo ndivyo Neno la Mungu lilivyo Kanisani, kile kinacholifanya Kanisa kuwa Bibi-arusi. Si dhehebu, hilo ni la Ibilisi, kila moja la hayo. Siwaiti watu walio mle ndani hivyo; hao ni maskini watu waliodanganyika, kama vile Yesu alivyosema, "Kipofu akimwongoza kipofu mwenzake." Naye asingeweza kuwaita watoke.

Nao wakasema, "Mbona, umezaliwa kwa uasherati! Ni nani anayekuambia, hapo, uje hapa? Ni shule gani, ni seminari gani iliyokutambua?" Kasema, "Sisi tunaye Musa. Tunajua …"

Akasema, "Kama mngalimjua Musa, mngalinijua Mimi."

Maana Musa alimwandika Yeye katika vitabu vyake vinne, "Bwana Mungu wenu atawainulia Mpaji wa Neno, Nabii mithili yangu, naye asiyemsikia Nabii huyo atakatiliwa mbali na watu." Hakuna lingine. Naye ni nini? Neno. Na ni kitu gani? Usiache chachu yoyote isalie kwenye … Usitie tu chachu miongoni Mwake. Usiongeze kanuni yo yote ya imani, madhehebu yo yote, kwa maana yamechafuliwa papo hapo, dhabihu yako imekwisha.

108 Hebu na tuharakishe sasa, upesi sana, ili mweze kwenda kula.

Angalia! Sasa, basi, wewe ni mwana wa Mungu, katika nyumba ya Mungu, wewe ni sehemu ya uchumi wa Mungu. Warumi 8:1, "Basi hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu." Kwa

maana wamekufa kwa ulimwengu, wako hai ndani Yake, na wanaishi katika siku hii ya leo, wakilifanya Neno ambalo Mungu amewatumia, ama kuwachagulia tangu asili, akayaweka majina yao katika Kitabu hiki cha Bibi-arusi. Na wakati Maji yanapokuja juu ya mbegu hiyo iliyo moyoni, huiinua ikawa Bibi-arusi wa Kristo. Loo, jamani! Ni kamilifu tu inawezavyo kuwa. Katika kila wakati imekuwa hivyo.

109 Walutheri, chini ya kuhesabiwa haki, miguu, waliinuka namna hiyo; Wesley, chini ya utakaso. Wapentekoste chini ya mikono, kazi na matendo na kadhalika, ilibidi wawe Wakalvini … ama ilibidi wawe Waarmenia, iliwabidi wawe washika sheria. Lakini sasa tunakuja kwenye kilele, lile jiwe la kifuniko. "Neema! Neema!" lile jiwe la kifuniko lililia.

Jiwe la kifuniko linalia nini? "Neema! Neema!" Kupita kutoka kwenye mauti na kanuni za imani, kuingia kwenye Neno lililo hai la Mungu aliye hai. Mpango pekee uliowekwa na Mungu kwa ajili ya wakati Wake, wanawe katika wakati wa Neno wamehuishwa na Roho kama vile spaki iliyowashwa kwa kitu fulani kuihuisha; na kuketi sasa katika ulimwengu wa roho (katika wakati uliopo), wakiwa hai tayari na watiifu kwa kila ahadi katika Neno. Basi hilo linafanya nini? Wewe ukiwa sehemu ya jeni ya Mungu, sehemu ya Neno, watu wengine sehemu ya Neno la Mungu, mmeketi pamoja, mnadhihirisha Mwili wote wa Kristo, kwa sababu hakuna chachu miongoni mwenu. (Ona kile anachozungumzia, Ndugu Brown?) Hakuna chachu miongoni mwenu, ni Neno tu, mmeketi katika ulimwengu wa roho, mlangoni mahali Yeye alipoliweka Jina Lake: Kristo Yesu.

110 Hakuna chachu miongoni mwenu, hiyo inaleta utimilifu wote wa uungu kwa jinsi ya mwili miongoni mwenu. Wasingefanya hivyo katika wakati wa Luther, wasingefanya hivyo katika wakati wa Wesley, wasingefanya hivyo katika wakati wa Kipentekoste; bali katika siku Mwana wa Adamu atakapodhihirishwa, kufunuliwa, kurudishwa Kanisani pamoja na Uungu wote wa Mungu miongoni mwa watu Wake, akionyesha ishara zile zile zinazoonekana, akijidhihirisha Mwenyewe kama alivyofanya hapo mwanzo wakati alipodhihirishwa duniani katika mfano wa Nabii-Mungu. Loo! Utukufu! Aliahidiwa na Malaki 4, aliahidiwa na Maandiko hayo mengine. Unaabudu wapi? Nyumba ya Mungu, umeketi (katika wakati uliopo).

111 Sasa, upesi, hebu tuangalie tu upesi sana sasa, kisha tuendelee kuhusu… Katika dakika kumi tutakuwa tumeondoka, Bwana akipenda.

Sasa hebu na tuwaangalie wengine ambao wamehuishwa katika nyumba hii ya Mungu, wa wakati wao.

Henoko! (Katika dakika kumi tutaondoka, kama mnaweza tu kuvumilia kwa muda huo zaidi.) Angalia, Henoko alikuwa Neno la Mungu lililo hai la wakati wake, yeye alikuwa ni nabii.

Nabii ni kiakisi cha Mungu. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Ki—kiakisi hakijiakisi chenyewe, ki—kiakisi sio uakisi. Kunapaswa kuwe na kitu kitakachokigonga kiakisi—kiakisi kukifanya kiakisi. Kwa hiyo nabii ni chombo teule cha Mungu ambacho hakiwezi kuakisi kitu cho chote ila yeye yuko sambamba moja kwa moja na uakisi huo, Mungu, kuakisi sura ya Kristo, Neno. Mnaona, hakuna kitu kingine kinachoweza kufanya jambo hilo. Wewe ni kiakisi, hiyo ndiyo sababu ilimbidi nabii kula hicho kitabu. Hiyo ndiyo sababu ilimbidi kula gombo. Ilimbidi kuakisi Neno hilo kwa ajili ya wakati huo. Mmelipata?

112 Angaliani Henoko, kiakisi kikamilifu wa Mungu katika mfano. Wakati Mungu alipomaliza—alipomaliza naye, Yeye alimhamisha tu, akamtwaa. Ile mitambo aliyokuwa ameiakisi ilifanyika nguvu tendaji pamoja na Roho, na ikampandisha juu.

Vivyo hivyo katika siku za Eliya. Eliya, hata kwenye mifupa yake, ambapo ule uakisi … Kiakisi cha Mungu katika mwili wake ukidhihirishwa Neno la Mungu. Waliilaza maiti ya mtu juu yake, akafufuka tena. Sisi ni nyama na mfupa Wake, mradi tu sisi ni Bibi-arusi wa Kristo. Unaamini jambo hilo? Vema. Yeye alitufia, nasi tulikufa kwa nafsi zetu na tumezikwa katika Jina Lake, ili kwamba "tusiwe tena wa ulimwengu, bali ndani Yake," ambapo jamii zote mbili za Mbinguni zinaitwa Yesu Kristo. Hiyo ni Waefeso 1:21. Kwa kuwa Mbingu … familia iliyo Mbinguni. Jamaa ya Mbinguni inaitwaje? Yesu. Familia iliyoko duniani inaitwaje? Vema, hiyo ndiyo nyumba ya Mungu ambamo mna ile Damu. Hiyo ni kweli? Huo ndio mlango, hilo ndilo lango, hapo ndipo mahali Yeye alipolikalisha Jina Lake, nalo Neno likafanyika mwili likakaa miongoni mwetu. Ni Neno likiakisi na kuuangaza wakati mnaoishi. Hivyo ndivyo Yeye alivyokuwa, hivyo ndivyo Musa alivyokuwa, hivyo ndivyo Yakobo alivyokuwa, hivyo ndivyo hao wengine walivyokuwa, wakiliangaza hilo Neno la Mungu, kiakisi ambacho Mungu alikuwa akijiakisia Mwenyewe. Ndipo kufikia ile sura kamili ya Mungu, Yesu Kristo, Kipeo cha Mungu; alipigwa apate kuwachukua hao wengine kama Bibi-arusi ambao wamekuwa ni viakisi.

113 Musa alikuwa ndani Yake. Yoshua alikuwa ndani Yake. Nawe kama uko ndani Yake, ulikuwa ndani Yake kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, familia ya Mungu; uliteswa pamoja Naye, ulikufa pamoja Naye, uliienda msalabani pamoja Naye, ulifufuka pamoja Naye; na sasa ungali pamoja Naye, umeketi katika ulimwengu wa Roho, ukiuakisia ulimwengu Ujumbe wa wakati huu, Nuru ya ulimwengu. "Ninyi ni Nuru ya Ulimwengu," lakini kama imefichwa na kikapu cha pishi la madhehebu, wataionaje? Kwa mapokeo

yenu, mnaitangua hiyo Nuru! Kwa kujaribu … Madhehebu yenu, mkijaribu kuizuia Nuru isiingie kanisani mwenu; hamwingii, wala hamuwaruhusu wao. Amina.

Hebu na tusimame tu. Jamani, nina mengi sana hapa. Tu—tungeweza kuendelea … Loo, jamani! Tunazo dakika tano.

114 Mnaona mlango ni nani? Mungu aliweka wapi Jina Lake? Katika Yesu. Unaingiaje katika Jina Lake? Unaingiaje mle? Kwa kubatizwa mle ndani! Vipi? Kwa maji? Kwa Roho! "Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja." Huo ni ubatizo wa Roho Mtakatifu.

Ubatizo wa maji unakuweka tu katika ushirika na watu, kwamba ulitambua ya kwamba umemkubali Kristo. Hiyo ni Kweli. Lakini ni ubatizo wa Roho. Ninaweza kuliitia Jina la Yesu juu yako na kukubatiza, hilo halilifanyi kuwa hivyo.

Lakini mara huyo Roho Mtakatifu kweli…Neno halisi linapoingia ndani yako (Neno, Yesu), basi, ndugu, Ujumbe si siri kwako basi; unaujua, ndugu, wote umeangaziwa mbele yako. Haleluya! Mungu asifiwe! Amina!

Nampenda, nampenda
Sababu alinipenda,
Na kununua wokovu wangu …

Mungu mpendwa, ninaomba ya kwamba utawaponya watu hawa, Bwana, na kumpa kila mmoja wao afya. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Loo! Upendo! Loo!

Tangu wakati huo, kwa imani nilipokiona kile kijito
Kilichosababisha majeraha yako, (kutoka kwenye kile Kipeo)
Upendo wenye kukomboa umekuwa ndio wimbo wangu,

115 Unawezaje … Mungu ni Upendo. "Yeye apendaye ni wa Mungu," upendo wa kiungu, mtakatifu, si upendo mchafu; upendo safi, safi, mtakatifu, upendo wa Mungu Neno. "Amri Zako nimezificha moyoni mwangu, nisije nikakutenda dhambi," loo, jamani, huyo ni Daudi akilia. Yeye si ni wa ajabu? Hivi hamumpendi?

Sasa, kuna Njia, Njia safi, takatifu, mahali pekee pa kukutania ambapo Mungu atakutana nawe. Si kwa sababu unasema, "Mungu, sasa, mimi ni Mmethodisti mzuri. Mimi ni Mbaptisti mzuri. Mimi ni Mpentekoste mzuri." La! Kwa sababu wewe uko katika Yesu Neno, sehemu ya Neno ambalo linadhihirishwa kwa siku hizi, Ujumbe wa siku hii; si wa Luther, wa Wesley, wa Kipentekoste; bali Yesu wako, ule uakisi, ambao umekuja katika *huu*. Huwezi kuurudia huo, huko ni kuongeza chachu kwenye Mkate wako mtakatifu, ambapo, "Mtu ataishi kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu, katika wakati Wake."

116 Ee njoo, Bwana Yesu, lile Jiwe kuu la Kichwa. Angalia mavumbi ya hao Walutheri waliokufa huko nyuma chini ya ufuia imani, yamewekwa pale; waangalie hao Wamethodisti.

Hao Wapentekoste na kadhalika, wanaojitokeza sasa, ule ukoo halisi uliotokea.

Ninyi Waassemblies of God mlijiundia madhehebu, wakati ni kitu kile kile ambacho Mungu aliwatoa kwake, mlirudi moja kwa moja kama vile nguruwe kwenye kugaagaa kwake.

Ninyi wa Umoja, wa United, maskini J.C. ya… Pentekoste Assemblies ya Yesu Kristo. Moja kwa watu weusi, nanyi mkajitenga kwa sababu ya ubaguzi. Ninyi mliofanya jambo hilo, kisha mkaungana wenyewe na kujiita "Umoja." Kisha mkaunda dhehebu, na kuwagombanisha Waassemblies: "Kama mbwa anavyoyaendea matapiko yake." Kama matapiko yalimchefua mbwa mara ya kwanza, hivi hayatamchefua tena? Badilisheni mlo wenu kutoka kwa madhehebu yenu mlirudie Neno, kisha muishi pamoja na Kristo. Aibu kwako!

Nina Baba ng'ambo kule,
Nina Baba ng'ambo kule,
Nina Baba ng'ambo kule,
Ng'ambo ile ya pili.
Siku moja angavu nitaenda kumwona,
Siku moja angavu … -enda kumwona,
Siku moja angavu nitaenda kumwona,
Kwenye pwani ya pili.
Loo, hivi huo hautakuwa mkutano wa furaha,
Hivi huo … (Neno linaenda kwa Neno!) mkutano, (Wakati Bibi-arusi anapopaa juu, Neno kwa Neno.) ... mkutano wa furaha,
Kwenye pwani ya pili.
Loo, siku hiyo angavu huenda ikawa ni kesho,

Siku hiyo angavu huenda ikawa ni kesho,
Siku hiyo angavu huenda ikawa ni kesho,
Kwenye pwani ya pili.

Mnasema, “Unamaanisha hilo, Ndugu Branham?”

117 Naam, bwana! Wakati Walutheri wa wakati huo, Waesley wa wakati wao, wapentekoste wa wakati wao (wale wa kweli, si wa kimadhehebu); Wapentekoste, wale walioongeza chachu (madhehebu yao), walikufa. Lakini Neno hili la kweli likisonga mbele, mnaona. Kama tu vile Yesu alivyosema, “Siku hiyo, mtajua ya kwamba Mimi niko ndani ya Baba na Baba yuko ndani Yangu, na Nami ndani yenu na ninyi ndani Yangu.” Yote ni Neno!

Loo, hivi huo hautakuwa ni mkuta-…wa furaha (wakati wanawe watakapokusanyika kwenye lango Lake)
… Mkutano wa furaha,
Huo hautakuwa mkutano wa furaha,
Kwenye pwani ya pili.

118 Sasa, kanisa, tunafundisha sasa. Lakini, kumbukeni, mtakapoondoka hapa, anzeni kuondoka kwenye kapi sasa; mnaingia kwenye punje, bali kaeni katika Uwepo wa Mwana. Msiongeze, yale niliyosema; usiondoe, yale niliyosema. Kwa sababu, ninanena Kweli kadiri nijuavyo Mimi, kama vile Baba alivyonipa. Mnaona? Msiongeze Kwake, semeni tu yale niliyosema.

Jambo ni kwamba, waambieni tu watu waje wamtafute Bwana Yesu. Na kisha ninyi nanyi mkae katika Uwepo Wake, mumpende tu, “Ee Bwana Yesu, Mwana wa Mungu, ninakupenda. Lainisha moyo wangu, Bwana. Ondoa uchafu wote na kuipenda dunia, na unijalie niishi mtakatifu katika ulimwengu huu wa sasa mbele Zako.”

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa maombi. Sasa, hebu tuone, tuna mtu yeyote aliyechaguliwa kuufunga mkutano kwa maombi? Ama, nitafanya hivyo, basi. Iweni na kicho kabisa.

119 Mungu mpendwa, tunakushukuru ya kwamba tumepata mlo wetu wa kiroho. Tunakushukuru, Bwana, ya kwamba vitamini ya Neno huwakuza wana wa Mungu. Haifanyi kazi na mtu mwingine yeyote, ila wana na binti za Mungu tu. Kwa hiyo tunakushukuru kwa ajili Yake. Nasi tunaomba, Mungu, ya kwamba tutapata faida mle, kwamba hatutakushukuru tu. Tunakushukuru kwa ajili Yake, bali hebu tutumie nguvu kujaribu kuninii (kwa Upendo) kuwashawishi watu wamwamini Mungu wetu; walio wakaidi, wenye dhambi, wanawake, wanaume, wavulana, wasichana, katika wakati huu.

Tukiona, Bwana, ya kwamba hali hii ya akili, wakati huu wenye wasiwasi ambao watu wanaishi, unawatia wazimu; kutimiza kabisa yale Maandiko yalisema na kuahidi, ya kwamba vitu vikuu vya kutisha vingekuja juu ya nchi; kama nzige, kuwatesa wanawake wanaokata nywele zao, watakuwa na nywele ndefu kama mwanamke. Na vitu mbalimbali vya kutisha ambavyo wataweza kuona, Bwana, katika hali walizo nazo za kiwazimu, zilizodanganyika, ndipo wataipigia makelele miamba na milima. Wanawake ambao wangewalea mbwa na paka, na wasiwalee watoto kukupa Wewe heshima. Hao uliowapa watoto nao wakawazaa, wanawaachilia mitaani wafanye watakavyo. Si ajabu Wewe ulisema, Bwana, ulipokuwa ukienda msalabani, “Ndipo wataanza kuililia miamba na milima iwaangukie.”

120 Tunaona kila kitu kingine kikisonga hadi wakati huu. Tunaona Maandiko yakithibitishwa, yakihakikishwa. Na wakati tu tunapoona Hilo, Bwana, Wewe kwa macho yetu wenyewe (ukidhihirishwa), siku moja kutakuwako na Unyakuo nasi tutaona dhihirisho la Neno hilo, “Kwa maana Mwana wa Adamu atakuja katika mawingu ya utukufu, na Malaika Wake watakatifu pamoja Naye, nasi tutatwaliwa juu kumlaki Yeye hewani.” Itakuwa basi … Tunasikia habari zake sasa, wakati huo tutayaona kwa macho yetu wenyewe.

Jalia tuonekane katika Yeye, Bwana, mahali pekee palipowekwa. Naye ndiye Sadaka. Tunamleta, yale tuliyosikia habari zake, Yesu Kristo, katika nyumba ya Mungu kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, kupitia Jina la Yesu Kristo. Na hapo Sadaka yetu inakubalika nasi tunaingizwa kwenye familia; kwa sababu, ingawa tunatangatanga ulimwenguni, tulichaguliwa wana na binti za Mungu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Asante kwa hilo, Baba. Loo, mtu yeyote angewezaje kuacha kitu kama hicho, wakati walipopata Ukweli, ya kwamba Mungu alikuwa amewachagua kutoka ulimwenguni? Kulikuwako na mamilioni waliopotea, siku ambayo niliokolewa.

121 Ee Mwana-Kondoo anayekufa, ninawezaje kukushukuru? Moyo wangu unawezaje kuwa na kicho cha kutosha mbele Zako? Nisaidie, Mungu mpendwa, kuishi mkweli. Wasaidie watu wangu kuishi wakweli. Ninawaombea, Bwana, kila mmoja, ya kwamba Wewe utaninii, Mungu, kwa namna fulani, si … Nisingejua jinsi … Sijui namna, namna tu ya kuomba, Bwana; na labda hata siombi jambo hilo kwa njia inayofaa. Bali samehe ujinga wangu, Bwana, na uuangalie tu moyo wangu. Ninaomba ya kwamba kusiwe na mmoja wao atakayepotea, si hata mmoja wao, Baba. Ninawadai, kila mmoja, kwa ajili Yako. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Nampenda, na …

Na kama mnampenda, pendaneni ninyi kwa ninyi. Peaneni mikono.

MESSAGE online hub
www.messagehub.info

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7